# MTINDO WA NYIMBO ZA INJILI ZA CHRISTOPHER NYANGWARA MOSIOMA (*EMBARAMBAMBA)* MWAKA 2021- 2023

**KIUNGA JONAH KESI**

TASNIFU HII IMETOLEWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA

CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA

Mount Kenya University

**MEI, 2025**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni ya uzamili katika chuo kingine.

Jina: Kiunga Jonah Kesi

Nambari ya Usajili: MAKI/2019/60098

Sahihi ……………………………… Tarehe: 25/06/2025

**Idhini**

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na chuo Kikuu cha Mount Kenya.

Msimamizi

Dkt. Jackline Njeri Murimi.

Chuo Kikuu cha Tom Mboya.

Sahihi:………………………… Tarehe: 27/06/2025

Mount Kenya University

**TABARUKU**

Natabaruku kazi hii nzima kwa mke wangu kipenzi Bi. Agnes M. Njeru na mwanangu Yness H.

Kesi kwa kunivumilia na kunipa  motisha katika kazi hii..

Mount Kenya University

# SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu Karima aliyenijalia mimi afya na siha njema kwenye shuhuli nzima ya kuafikia umbali huu wa masomo. Ama kweli yeye ni EBENEZA.

Pili naishukuru familia yangu, mke wangu na mwanangu kwa kunivumilia na kunipa muda mwingi wa kuwa mbali nao ili niendeleze masomo yangu na kufanikisha Tasnifu hii.

Tatu, ningependa kumshukuru msimamizi wangu Dkt. Jackline Njeri Murimi ambaye hakuchoka kunielekeza na kunirekebisha usiku na mchana kwenye shughuli nzima ya kufanikisha hili.

Nne na mwisho, nashukuru sana Chuo Kikuu cha Mount Kenya na idara husika kwa kunikubalia kuendeleza masomo yangu na hata kufanikisha utafiti wangu na kunisaidia kufika umbali huu wa masomo.

## IKISIRI

Nyimbo ni moja wapo wa tanzu za Fasihi zinazopatikana miongoni mwa wanajamii. Kuna mifano mingi ya aina ya nyimbo za dini zinazotumika katika shughuli mbalimbali za kuabudu na kumtukuza Mungu. Nyimbo hizi zina majukumu muhimu yanayoendana na mambo ya dini, haswa za shughuli za ibada. Katika hali ya kawaida, nyimbo hutungwa kwa ustadi wa kiwango cha juu cha lugha. Tasnifu hii imejadili mtindo katika kuwasilisha ujumbe kwenye nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma msanii wa nyimbo za injili nchini Kenya almaarufu *Embarambamba*. Utafiti huu umeainisha, kutambulisha na kufafanua vipera vya kimtindo vinavyotumiwa na mwanamuziki Christopher Nyangwara Mosioma anapotunga nyimbo zake na pia kuangazia maudhui ambayao huambatana moja kwa moja na mtindo anaoutumia msanii kwenye kuumba kazi yake. Utafiti huu umejikita katika vipengele vinne; mtindo, msuko, maudhui na matumizi ya lugha. Utafiti huu ulilenga kufanikisha lengo moja kuu na malengo matatu maalumu ambayo ni; Kuainisha msuko wa maudhui, Kuchanganua matumizi ya lugha na la mwisho ni kutathmini athari za mtindo wa msuko wa maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za injili za Christopher Nyagwara Mosioma (*Embara mbamba)* mwaka 2021- 2023. Maswali ya utafiti yalikuwa; Je, ni maudhui yapi yanayopatikana katika nyimbo za Christoppher Nyangwara Mosioma? Ni mtindo upi wa matumizi ya lugha unaojitokeza katika nyimbo za injili za Christopher Nyangwara Mosioma? Na je, mtindo wa msuko wa maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma una athari gani katika jamii? Nadharia iliyotumika ni Nadharia ya Simiotiki inayojishughulisha na ishara pamoja na hali ya kuashiria kwenye utunzi wa Fasihi. Uteuzi wa sampuli kimaksudi ulitumika katika ukusanyaji wa data. Data yenyewe ilinakiliwa kwa kurejelea malengo ya utafiti na msingi wa nadharia husika. Utafiti wa maktabani ulitumika kwa ukusanyaji wa data kwa kusoma tasnifu za awali, vitabu na matini za mtandaoni ambazo zilisaidia kuafikiwa kwa malengo ya kazi hii. Matokeo ya utafiti huu yameandikwa kwa kufuata muundo wa wa kimaelezo. Data yenyewe ilikusanywa kwa njia moja kuu ya usikilizaji makini wa nyimbo husika za msanii teule na kudondolewa kwa vipengele vinavyohitajika na kuandikwa. Umuhimu wa utafiti huu ni kuwa, wasanii watanufaika pakubwa katika kuzijenga kazi zao za kisanii kwa weledi na ufundi mkubwa na hata matokeo ya kazi hii pia, yatatumika kama moja wapo ya vipengele yva kubainisha pengo la maarifa litakalojazwa na utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu pia yatawafaa pakubwa watafiti na wasomi kwa kupata marejeleo katika uwanja huu wa utafiti huu uliofanywa.

Mount Kenya University

**ABSTRACT**

Songs are one of the very important categories of oral literature in our society. Among them, there are worshipping songs that praise God. There are various types of religious songs that are used in various purposes of praising and worshipping God.These songs have important purposes that bound themselves in the religion, esprcially religion functions. Generally songs are well composed and involve various stylistic devices. This research was meant to examine the style involved in the sending of message in the songs of Christopher Nyangwara Mosioma, a Kenyan Gospel artist also known as *Embarambamba.* Song composing as in other forms of literature involves complex styles in order to drive home the intended message to the audience. This research has therefore identified, described and evaluated the different stylistic devices that Christopher Nyangwara Mosioma used in composing his songs and which from them we identified the themes got in the songs. The research was about three aspects: stylistic device, formation of themes and grammar usage. The research questions were as follows: which themes are in the songs of Christopher Nywangwara Mosioma? Which stylistic devices are in the songs of Christopher Nywangwara Mosioma? What effects does the style of formation of theme and grammar usage in the songs of Christopher Nyangwara Mosioma have in the society? The research had one main objective and other specific three objectives: To Explain the themes formation, To discus the grammar usage and the last one was to Evaluate the effects of the style of formation of themes in the songs of Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*) in the year 2021-2023. Purposeful sampling was used in the data collection. The research data was analysed basing on the research objectives and the theory used. The theory that was used in this research was the Semiotic theory that was initiated by Ferdnand Dessaussure. The data of the research was collected through reading of books, journals, Swahili dictionary, other researches and internet publications related to the the research topic. The research methodology involved one major method of collecting data, where the targeted songs were keenly listened and the needed key elements were recorded. This research will be greatifully useful to artists in their whole process and steps when composing and writing their work. What the project is puting forward will fill the gap that was there before this piece of work was completed. Further more the work done in this research will provide scholars and educators with reference materials on matters and fields related to this work.

Mount Kenya University

# YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ........ ii
TABARUKU ........ iii
SHUKRANI ........ iv
IKISIRI ........ v
ABSTRACT ........ vi
YALIYOMO ........ vii
ORODHA YA MAJEDWALI ........ x
UFUPISHO ........ xi
SURA YA KWANZA ........ 1
MSINGI WA UTAFITI ........ 1
**1.0 Utangulizi** ........ 1
**1.1 Usuli wa Utafiti** ........ 1
**1.2 Suala la Utafiti** ........ 5
**1.3 Malengo ya Utafiti** ........ 5
**1.4 Maswali ya Utafiti** ........ 6
**1.5 Sababu za Kuchagua Mada.** ........ 6
**1.6 Umuhimu wa Utafiti** ........ 7
**1.7 Upeo na Mipaka** ........ 8
**1.8 Maelezo ya Istilahi zilizotumika** ........ 8
**1.9 Hitimisho** ........ 9
SURA YA PILI ........ 10
MWAUO WA MAANDISHI ........ 10
**2.0 Utangulizi** ........ 10
**2.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mada** ........ 10
**2.2 Misingi ya Nadharia** ........ 16
**2.3 Hitimisho** ........ 19
SURA YA TATU ........ 20
MBINU ZA UTAFITI ........ 20
**3.0 Utangulizi** ........ 20
**3.1 Muundo wa Utafiti** ........ 20

Mount Kenya University

**3.2 Sampuli na Usampulishaji** ........ 20
**3.3 Mbinu na Vifaa vya kukusanya Data** ........ 21
**3.4 Uchambuzi na Uwasilishaji wa Data** ........ 22
**3.5 Maadili ya Utafiti** ........ 23
**3.6 Hitimisho** ........ 23
SURA YA NNE ........ 25
UCHANGANUZI WA DATA NA UFASIRI WA MATOKEO YA UTAFITI ........ 25
**4.0 Utangulizi** ........ 25
**4.1 Historia fupi ya Christopher Nyangwara Mosioma** ........ 25
**4.2 Muhtasari wa Kazi za Mziki za Christopher Nyangwara Mosioma** ........ 25
**4.3 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti** ........ 26
**4.4 Maudhui katika Nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambama*) katika Mwaka wa 2021-2023** ........ 26
**4.4.1 Maendeleo ya Kiuchumi** ........ 26
**4.4.2 Ulokole** ........ 29
**4.4.3 Imani ya Kidini** ........ 32
**4.4.4 Ukuu wa Mungu** ........ 35
**4.5 Mtindo wa Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*) katika Mwaka wa 2021-2023** ........ 39
**4.5.1 Takriri** ........ 40
Jedwali 4.1: Maneno Yaliyotakririwa ........ 41
**4.5.2 Kuhamisha Msimbo** ........ 44
Jedwali 4.2: Maneno yaliyohamishiwa Msimbo ........ 44
**4.5.3 Kuchanganya Ndimi** ........ 45
**4.5.4 Tashbihi** ........ 46
**4.5.5 Unukuzi kutoka Vitabu Takatifu** ........ 48
**4.5.6 Sitiari** ........ 50
**4.5.7 Jazanda** ........ 51
**4.5.8 Usimulizi** ........ 53
**4.5.9 Uteuzi wa maneno** ........ 58
**4.6 Athari za Mtindo wa Msuko wa Maudhui na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma** ........ 65
**4.6.1 Athari Chanya kwenye Mtindo wa Msuko na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma ni kama zifuatazo:** ........ 67

Mount Kenya University

**4.6.2 Athari Hasi kwenye Mtindo wa Msuko na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma ni kama zifuatazo:** .................... 70
**4.7 Hitimisho**.................... 80
SURA YA TANO.................... 81
MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO .................... 81
**5.0 Utangulizi**.................... 81
**5.1 Muhtasari**.................... 81
**5.2 Mapendekezo**.................... 84
**5.3 Hitimisho**.................... 85
MAREJELEO .................... 86
VIAMBATANISHO.................... 91
Kiambatisho I : Barua ya idhini ya chuo (ERC) .................... 91
**Kiambatanisho II: Idhini ya Utambulisho**.................... 92
Kiambatanisho III: Barua ya Idhini (NACOSTI). .................... 93
**Kiambanatisho IV : Ripooti ya Turtin**.................... 94

Mount Kenya University

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 4.1: Maneno yaliyotakririwa.................................................................................. 42

Jedwali 4.2: Maneno yaliyohamishiwa Msimbo ................................................................ 45

Mount Kenya University

# UFUPISHO

TUKI – Taasisi ya Uchunguzi ya Kiswahili.

Uk – Ukurasa

Bi – Bibi

Bw – Bwana.

DOK – Depth of Knowledge (Kina cha Maarifa)

Mount Kenya University

# SURA YA KWANZA
# MSINGI WA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sehemu hii inaelezea kuhusu usuli na suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu, upeo na mipaka ya utafiti na kumalizia na maelezo ya istilahi kama yalivyotumika katika kazi hii.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Jumuiya ya muziki ulimwenguni inaendelea kukua na kuwajenga wasanii kiafya na hata kiuchumi. Mziki wa injili ulimwenguni unaotungwa na wanamziki wa kisasa umesheheni mawimbi ya kimapinduzi kutokana na njia ya uwasilishaji wake. Mapinduzi haya yanaweza kuchukuliwa kuibua changamoto nyingi za kimaadili na kidini. Jambo hili linafaa kutiliwa mkazo mno kwenye kazi za wanamuziki ili wadumishe ubunifu wa kisasa na bado wajikite kwenye ujumbe uliosheheni mambo ya Kristo. Baadhi ya wasanii tajika wa nyimbo za injili ulimwenguni ni kama Kirk Franklin, Don Moen, Cece Winams na Lecrae kutoka nchi ya Marekani.

Tunapoangazia mtindo wa mziki wa injili barani Afrika tunabaini mabadiliko mengi ambayo yameendelea kutokea kwa miaka mingi ukiathiriwa mno na mafunzo ya tamaduni za kiafrika, kanuni za dini ya kikristo na hata mitindo mingine zaidi ya muziki wa kisasa na mingine ya kimataifa. Mitindo maarufu ya muziki wa injili barani Afrika ni kama: Gospel ya Kiasili (Traditional African Gospel), Urban Gospel, Gospel HipHop (Rap Gospel), Afro-Gospel, Gospel Choir (Praise and Worship), na Gospel Reggae.

Kutokana na haya ni wazi kwamba mtindo wa muziki wa injili barani Afrika umejaa utajiri mwingi wa miondoko tofauti na unaendelea kubadilika. Jambo hili linawafanya wasanii kujaribu kuwafikia watu tofauti tofauti wa rika mbalimbali huku wakijaribu kuegemea mitindo ya muziki wanayoipenda na kuhifadhi ujumbe wa Kikristo. Wasanii wa nyimbo za injili barani Afrika wanaofanya vizuri ni pamoja na: Sinach, Mercy Chinwo na Nathaniel Bassey wa kutoka Nigeria,

Mount Kenya University

Pompi wa nchini Zambia, na hata Christina Shusho wa Tanzania. Wasanii hawa wameekeza katika kazi zao kwa bidi kubwa kwenye kuieneza injili kupitia muziki kwa viwango vya juu katika kanisa, redio, You-Tube na hata majukwaa ya kimataifa. Na kwa pamoja wamefaulu kuwa daraja la kuunganisha kizazi cha zamani na kizazi kipya, huku wakibaki waaminifu kwa ujumbe wa kiinjili.

Nyimbo za injili nchini Kenya zimekuwa maarufu mno kutokana na jinsi zinavyowavutia wasikilizaji. Wasanii wa nyimbo za injili nchini Kenya wameongezeka mno wakiwemo: JaBidii, Solomon Mkubwa, Size 8 Reborn, Embarambamba na marehemu Anjela Chibalonza. Katiba yetu nchini Kenya katika sura ya pili kifungu cha kumi na moja imepambanua masuala mbalimbali kuhusu utamaduni, kwamba, taifa litaimarisha uelewano, kuvumiliana na kukubali tofauti zilizoko miongoni mwa tamaduni za makabila yote nchini: kwamba, taifa litahifadhi, litalinda na kuimarisha turathi za Kenya – na hasa kuhusiana na utamaduni, historia, dini, maeneo ya historia chimbo na vifaa chimbo; kwamba, taifa  litakuza sanaa zote za kitaifa na kiutamaduni kwa njia ya fasihi, sanaa za maonyesho, uchoraji na uchongaji.

Kama ilivyo katika shughuli nyingi za kitamaduni, matumizi ya nyimbo yanahusishwa sana kwenye matukio ya kitamaduni. Ikumbukwe kwamba katika kudumisha na hata kupitisha tamaduni hizi kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine, nyimbo huchukua nafasi ya kwanza katika kufanikisha dhima hio. Ni katika nyimbo ambapo watu huburudika, huelimika na hata kupunguza mawazo na machovu yanayotokana na siku nzima ya mahangaiko ya kutafuta riziki.

Kuna aina mbali mbali za nyimbo zikiegemea shughuli za kijamii za kila siku. Kuna nyimbo za jandoni, nyimbo za nyiso, nyimbo za bembezi, nyimbo za mbolezi, nyimbo za dini na nyinginezo. Katika kuzitunga nyimbo hizi sharti pawepo na mtindo fulani unaofungamana na weledi alionayo mtunzi wa nyimbo husika.

Mount Kenya University

Kazi nyingi za kisanii huhusisha mtindo katika uwasilishaji wake. Wamitila 2008, anaelezea mtindo kama sifa bainifu za utunzi wa kazi ya fasihi ambazo humtofautisha mtunzi husika na watunzi wengine ukirejela upekee wa kazi yenyewe. Mtindo unaweza kubainishwa na vipengele kadhaa vikiwemo usimulizi na hata matumizi ya lugha.

Kutokana na maelezo haya, tasnifu hii imejikita katika kuchanganua mtindo kwa kuegemea upande wa matumizi ya lugha ya kisanaa kama kipengele moja wapo cha mtindo kwenye ujenzi wa maudhui yanayopatikana katika kazi ya fasihi.

Katika mtiririko, msuko huwa umefumwa katika mifumo ya kila aina kulingana na utanzu wa mtunzi aliokusudia kujikita nao. Nikitolea mfaano wa mpangilio wa visa na matukio katika fasihi andishi hasa katika uandishi wa Tamthilia na Riwaya ambapo matukio na visa vyake hutokea kiusababishi na kwa sababu hio hujulikana kama ploti. Katika kazi za kishairi msuko ndio unaorejelewa kama muundo ambapo mpangilio wa vina, mishoro na beti ndio unaleta athari kupitia muwala wa kazi yenyewe. Muwala ni upatanifu au uwiano mzuri wa vipengele vyote vya shairi.

Kazi ya fasihi hutumia lugha kwa namna fulani na tofauti ili kuweza kufanikisha matokeo yaliyokusudiwa na mwandishi au msanii kwa msomaji au msikilizaji wa kazi yake. Hiki ni kipengele muhimu cha kimtindo kinachoweza kumtofautisha mwandishi au msanii kwa wandishi au wasanii wengine hata iwe ni kwenye utanzu sawa. Katika kipengele hiki nyenzo mbalimbali za lugha hutumiwa; hizo ni kama tamathali za usemi na mbinu nyingine za kisanaa. Matumizi ya lugha katika kazi za kifasihi ina aina kadha kutokana na mwandishi au mtunzi na jinsi ambavyo amechagua kuwasilisha maudhui. Kupitia lugha mtunzi anaweza kutumia uteuzi na mpangilio wa

msamiati, tamathali za usemi, mbinu nyingine za lugha, jazanda, uhusishi (maana husishi) na unasibishi (maana nasibishi), methali na semi (Wamitila 2008, uk, 365-369).

Kulinga na Materu anafasiri nyimbo kama aina ya ushairi ambao huimbwa na hata unaweza kuhusisha kucheza kwa waimbaji wake na pia kuhusisha matumizi ya ngoma. Pamoja na haya yote anaongozea kusema kuwa lazima lugha ya nyimbo iwe ya kisanaa na inayojihusisha na mambo ya kijamii.

Katika mziki wa injili nchini Kenya kwa jumla kuna mambo kadhaa ambayo msanii wa mziki huu anafaa kuyazingatia ikikumbukwa kwamba kazi yake inalenga watu wanaoamini uongofu na mambo yaliyonyooka kimaadili. Aghlabu nyimbo husheheni dhima ya kuadilisha, kuelimisha na hata kudumisha maadili na historia ya jamii kulingana na miktadha mbalimbali. Nyimbo hizi zinafaa kuwa na maneno yaliyoteuliwa kwa uangaliifu na kwa ustadi mkubwa ili kuboresha na kuhifadhi heshima baina ya wasikiliaji wenyewe kwa wenyewe na hata msanii husika.

Ikumbukwe kwamba sifa moja wapo ya nyimbo za injili ni ile ya kubeba maneno yanayosifu Mungu kwa asilimia kubwa na maudhui mengine ya kutahadhari na kujitayarisha kuja kunyakuliwa na bwana Yesu. Fauka ya hayo nyimbo hizi zinafaa kwa ukawaida kusikilizwa katika nyumba za ibada na mihadhara ya ibada ambayo inahusishwa sana na uwepo wa Mungu na kuwa mahali patatifu kulingana kaida za mazingira haya.Hadhira inapoipokea kazi hii inatarajiwa kuwajaza upako na hata kuwasogeza karibu na uwepo wa Mungu.

Kwa maelezo haya, tasnifu hii ilitathmini mtindo wa msuko wa maudhui unaopatikana kwenye matumizi ya lugha katika nyimbo za injili za msanii Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba)*, kwani nyimbo hizi zimekuwa zikiangaziwa sana mitandaoni kwa kuzua hisia mseto miongoni mwa wanajamii.

## 1.2 Suala la Utafiti

Kama anavyoeleza Wamitila 2008, kwamba mtindo kama sifa bainifu za utunzi wa kazi ya fasihi humtofautisha mtunzi husika na watunzi wengine ukirejela upekee wa kazi yenyewe. Mtindo unaweza kubainishwa na vipengele kadhaa vikiwemo usimulizi na hata matumizi ya lugha.

Hivi karibuni msanii Christopher Nyangwara Mosioma amekuwa akiangaziwa sana kwenye mitandao kwa sababu ya nyimbo zake zinazoleta ukinzani wa kile anachoimba haswa. Ni katika mchakato huu mzima ulionipelekea kuzamia kwa kina katika kuangazia mtindo anaoutumia katika nyimbo zake msanii kwani ni katika mtindo ambapo msanii anaweza kueleweka vyema anacho maanisha au hata kuchukuliwa kupotosha maadili kilingana na kazi yake husika.Tasnifu hii ilihakiki mtindo alioutumia mwimbaji wa nyimbo za injili Christopher Nyangwara Mosioma katika kusuka na kuupenyeza ujumbe wake, hasa akiutumia mtindo huo bainifu kwenye nyimbo zake na hata kuzua ufaafu wa kukubaliwa au kukataliwa na hadhira lengwa.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Kazi hii iliongozwa na lengo moja kuu na malengo mengine matatu maalumu.

Lengo kuu lilikuwa ni Kuchanganua mtindo wa nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*) mwaka 2021-2023.

Katika kuafikia lengo hili, malengo mengine matatu maalumu yafuatayo yalishuhulikiwa:

i. Kuainisha msuko wa maudhui katika nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*), kama lengo kuu la utafiti.

ii. Kuchanganua matumizi ya lugha ya kisanaa katika nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*) mwaka 2021- 2023.

iii. Kutathmini Athari za mtindo wa msuko wa maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za Christopher Nyakwara Mosioma (Embarambamba).

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Kazi hii ilijibu maswali ya utafiti matatu ambayo yametokana kwa ukaribu na malengo yanayoongoza utafiti husika:

i. Je, ni maudhui yapi yanayopatikana katika nyimbo za Christoppher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*)?

ii. Ni mtindo gani wa matumizi ya lugha ya kisanaa yanayojitokeza katika nyimbo za injili za Christopher Nyagwara Mosioma (*Embarambamba*)?

iii. Je, ni athari zipi zinazojitokeza kutokana na mtindo wa msuko wa maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma (Embarambamba).

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada.

Nyimbo za injili mara nyingi zinafungamanishwa na shughuli za kumtukuza Mwenyezi Mungu. Tangu jadi nyimbo hizi zinabebeshwa majukumu ya kidini katika kuimbwa na hata kwenye mitindo ya kudensia. Maneno ya nyimbo hizi husika pia huteuliwa kwa uangalifu wa hali ya juu ili kuzua tu yale ambayo yanapaswa kuzuka kwenye shughuli za ibada. Masuala yanayofungamana na ibada yanachukuliwa kuwa ya kiungu na matakatifu, yaliyosheheni utakatifu na unyenyekevu mbele za Mwenyezi Mungu.

Nyimbo hizi za injili hujengwa na kuimbwa na watu walio na umri tofauti tofauti na kamwe hazina sharti la kutengewa umri wala rika fulani zinapoimbwa. Ikumbukwe kwamba, panapokuwa na ibada watu wa umri tofauti tofauti hukongamana pamoja na kushiriki bila kubaguana kwenye kusuduo la kumuabudu Mungu. Hakuna vizuizi vyovyote ambavyo huzuka panapotokea haja ya kuimbwa nyimbo zinazochukuliwa kuwa ni za injili.

Katika kuangazia nyimbo za injili za msanii Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*) pamekuweko na vizuizi na tahadhari katika kuzicheza na hata kuziimba nyimbo zake kwenye shughuli za ibada. Hivi karibuni baraza la kuangazia maadili kwenye Sanaa nchini Kenya lilipiga marufuku nyimbo fulani za msanii huyu husika kutoskizwa na hata kuchezwa kwenye vyombo vya habari. Katika kusikiliza kwa makini nyimbo za msanii huyu, maneno ya kumuabudu Mungu yanajitokeza kwenye nyimbo zake hata kwenye wimbo wake uliopigwa marufuku wa *Nataka Kunyonywa*.

Kazi hii imenuia kudhihirisha wazi mtindo alioutumia msanii husika kuumba nyimbo zake na kujaribu kujibu maswali husika ambayao yanazuka kwenye kujua kwanini nyimbo za msanii zinaibua kupigwa marufuku na hata kuwa mwiko kusikizwa kwenye majumba ya ibada. Utafiti huu pia utasaidia katika kuiweka jamii kwenye uelewa wa utunzi wa nyimbo na kwenye kuteua msamiati unaofaa kwenye kuumba kazi za kisanii. Utafiti huu pia unanuia kuziba mapengo ambayo yako wazi kwenye kutafiti mtindo unaopatikana kwenye nyimbo katika jamii.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unanuiwa kuwa na manufaa kadha wa kadha tukitanguliza manufaa ya kuziba kwa kiasi kikubwa pengo lililopo hasa ikizingatiwa kwamba hakuna tafiti zingine ambazo zimechunguza mtindo wa msuko wa maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za msanii husika. Ni katika kuchunguza mtindo wa kuumba nyimbo za msanii huyu husika ambapo uteuzi wa msamiati bainishi ndio unaojenga kile kilicholengwa. Utafiti huu umeweka wazi mchakato mzima wa kuteua na hata matumizi ya msamiati teule kwenye kuziumba nyimbo katika jamii. Hatua hii itamwezesha mwanajamii kuelewa kwa uwazi nyimbo za msanii husika kwani hakuna utafiti mwingine uliofanywa kumhusu unaoangazia kipengele hiki.

Utafiti huu pia utatumika kama mojawapo wa vyombo vya marejeleo kwa tafiti zingine zitakazoendeleza sehemu nyingine ya utafiti huu. Mambo ya kutafiti katika nyimbo za msanii huyu ni mengi na utafiti huu utatumika kama nguzo ya kuegemea kwenye kuendeleza tafiti zingine zitakazomuhusu msanii huyu au hata nyimbo zake.

Hali kadhalika utafiti huu utawafaa pakubwa wasanii katika kuzijenga kazi zao za kisanii kwa weledi na ufundi mkubwa. Na kwa kiasi kikubwa, matokeo ya utafiti huu yatatumika kama moja wapo ya vipengele yva kuweka wazi pengo la maarifa litakalojazwa na kazi hii kwani ujenzi wa kazi unahitaji umakinifu wa kimtindo na kutilia maanani hadhira lengwa. Kazi hii kwa jumla itatumika kama sehemu ya marejeleo kwa watafiti na wasomi watakaojihusisha na mambo yanayohusiana na kazi hii usoni.

## 1.7 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulijikita katika fasihi simulizi kwenye kipera cha nyimbo. Nyimbo zenyewe ni za kidini zinazojulikana kama nyimbo za injili. Nyimbo zinazotafitiwa ni nyimbo zilizoimbwa na msanii Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*) mwaka 2021- 2023 ambazo zinafika takriban nyimbo kumi na moja. Utafiti uliojikita kwenye mtindo wa utunzi katika kazi zake na kuongozwa na mihimili ya Nadharia ya simiotiki.

## 1.8 Maelezo ya Istilahi zilizotumika

**Nyimbo za Injili:** Ni aina ya nyimbo ambazo wakristo huziimba katika shuhuli zao za kusifu na kumuabudu Mwenyezi Mungu.

**Weledi:** Kiwango fulani cha ujuzi alionao msanii kwenye kubuni kazi zake za fasihi.

**Msuko:** Ni mbinu ambayo msanii huitumia kuunganisha vijenzi mbalimbali vya kazi ya kisanaa ili kufanikiwa kuupitisha ujumbe kwa hadhira yake yaani huwa ni mpangilio na mtiririko wa visa na matukio.

**Mtindo:** Ni njia fulani ya uwasilishaji wa kazi ya kisanaa ambayo msanii huitumia ili kuuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake.

**Matumizi ya Lugha:** kwa maelezo ya kifasihi, ni namna lugha ilivyotumika kwa jumla katika kazi husika kwa madhumuni ya kupitisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

**Lugha ya Vijana**: msamiati maalum unaotumiwa na watu walio wa rika moja wenye umri kati ya miaka 20-40.

### 1.9 Hitimisho

Sura hii imeeleza masuala kuhusu utafiti unaokusudiwa kufanywa yakiwemo: usuli wa utafiti ambapo ulihusu mtindo wa nyimbo za msanii husika ukiegemea matumizi ya lugha ya kisanaa. Kisha ikaangazia suala la utafiti ambalo lilihusu kwa mapana mtindo bainishi ambao msanii husika anautumia kuumbia kazi zake na kisha kuangazia tatizo la utafiti na malengo teule ya kazii hii. Maswali ya utafiti pia yaliangaziwa na kwa jumla yalikuwa maswali matatu ambayo pia yalieleza umuhimu wa utafiti huu kwa sehemu yake. Mipaka ya kazi yenyewe imebainishwa wazi katika sura hii na hata kueleza maana ya istilahi zote zilizotumiwa humo. Ili kupata msingi bora wa mada ya utafiti sura ifuatayo ya Mwauo wa Maandishi itatazama kwa kina kazi za tafiti na maandishi mbali mbali yaliyotangulia.

Mount Kenya University

# SURA YA PILI
# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi

**Sehemu hii inazungumzia kwa undani mapitio ya maandishi yanayoelezea dhana ya nyimbo na** uchambuzi wake, mtindo, msuko, maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo na hata kugusia nadharia iliyoongoza utafiti husika.

## 2.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Katika utafiti wa Finnegan wa 1970 kuhusu umuhimu wa nyimbo katika jamii za Afrika anazitaja nyimbo za siasa kuwa ni muhimu sana katika vipera vya nyimbo. Katika utafiti wake huo, Finnegan aliegemea na kutumia nadharia ya Mageuzi. Anasema kwamba nyimbo nyingi za kiafrika huleta umuhimu kutokana na mtindo na maudhui yake ambayo hutoa mwongozo katika jamii. Finnegan alibainisha wazi namna ambavyo dhima hujitokeza katika nyimbo za Afrika mashariki na kati. Utafiti wake uliufaa kwa kiasi fulani kazi hii kwa kuwa ulituchangia kufahamu maudhui kwenye nyimbo za Kiafrika ilhali utafiti huu utajikuta katika kuchanganua mtindo anaoutumia msanii Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba)* katika kuuwasilisha ujumbe wake kwenye nyimbo zake.

Nkonge (1988), alitafiti kuhusu mtindo na maudhui katika nyimbo za Joseph Kamaru. Kazi yake inaangazia kwa ujumla mtindo anaoutumia msanii husika na maudhui yanayojitokeza katika nyimbo zake. Alibaini maudhui katika nyimbo za msanii husika hasa akiangazia mtindo ambao aliutumia kwenye kutuga nyimbo zake, mtindo huo ndio ulimuwezesha Nkongwe kuweza kubaini maudhui yanayopatikana kwenye nyimbo za Joseph Kamaru kiurahisi kabisa. Kazi yake iliifaa hii katika kutambua mtindo na hata kuchanaganua maudhui yanayopatikana kwenye nyimbo za msanii Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*).

Kulingana na uchanganuzi wa Kieti (1989), kuhusu taswira na mazingaombwe katika kuuwasilisha ujumbe wa mwimbaji, anadai kwamba majina yao yaliundwa kimafumbo. Kieti alifafanua jinsi majina wanayopewa wahusika huwa na maana fiche na hata kuleta dhana ya uhuishaji kutokana na majina yenyewe. Majina haya mara nyingi hupewa wanyama huku yakirejelea sifa za kimadamu ili kuweka wazi uwezo walionao kwenye mazingaombwe. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na hii kwa sababu hii ilihusisha nyimbo za kisasa. Hata hivyo kama alivyoeleza Kieti (1989) mtindo wa kuwapa wahusika majina kulingana na tabia zao ni mbinu ya ulinganishi ambayo imeisaidia sana kazi hii na kuiteua kama njia moja yapo ya kimtindo katika nyimbo za msanii anayetafitiwa.

Kutokana na kazi za Ntarangwi (1990), akitafiti kuhusu maudhui katika nyimbo za Remi Ongala na Yalwala (1991), akiangazia maudhui katika nyimbo za John Mwale, tutatusaidika pakubwa katika kulenga shabaha ya kuchambua maudhui katika nyimbo za msanii wetu husika. Kulingana na wawili hawa maudhui ya nyimbo hubainika zaidi na kwa njia ya uwazi pale mtu anapojikita kwenye mtindo wa uwasilishaji wa nyimbo zenyewe. Maudhui yenyewe huchipuka kwenye fani na tamathali za lugha zilizotumiwa kuziumba kazi husika. Ijapokuwa wawili hawa walitafiti nyimbo za wasanii wawili tofauti, utafiti wao uliufaidi utafiti huu kwa sababu mojawapo ya malengo ya utafiti huu ni kuhusu uhakiki wa maudhui. Utafiti wa wawili hawa uliusaidia huu kwenye kuangazia mtindo n ahata kupata maudhui kwenye nyimbo zilizolengwa na kazi hii.

Katika maelezo ya Kimani na Chimerah (1999:21-23), kuhusu maudhui, wanasema kwamba ni ujumbe wa dhana ya matukio unaohusu viumbe waliobuniwa na mtagusano wa hali ya maisha kama yanavyojidhihirisha kwenye kazi za fasihi. Wanaongeza kwa kusema kwamba mwingiliano wa mada na maudhui ndio unaoleta msuko katika kazi ya msanii. Maelezo haya ya Kimani na Chimerah yalitufaa sana katika utafiti wetu kwenye kuchambua maudhui yanayopatikana katika

nyimbo za *Embarambamba* na hata kuelewa na kupambanua msuko wa matumizi ya lugha kwenye kuziumba nyimbo lengwa za kazi hii.

Wambua (2001), alionyesha uhusiano unaopatikana kwenye maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo pale alipotafiti vipengele vya kimtindo na maudhui katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Waambua alifafanua kwa uwazi ukaribu na mahusiano yaliyopo baina ya matumizi ya lugha na uhakiki wa maudhui katika kazi ya fasihi. Alitaja uhusiano uliopo katika fani na tamathali ili kubaini ufaafu wa kimaana katika kuzitafsiri nyimbo. Utafiti wa Wambua ulifaa utafiti huu kwani utafiti wetu umejikita pia kwenye lugha na maudhui ambapo kwenye kubaini na kuichambua lugha iliyotumiwa, ndipo tafsiri za nyimbo zilizolengwa na kazi hii ziliwezeshwa kufanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Katika utafiti wake Traore (2002), kuhusu nyimbo za taarabu za asili ya Zanzibar, alibainisha jinsi nyimbo za taarabu zilivyoendeleza na kudumisha kwa kiasi kikubwa mila na utamaduni wa Waswahili. Kwa kiasi kikubwa Traore kama walivyofanya watafiti wengine wa hapo jadi, aliangazia sana maudhui na kuipa kisogo sehemu inayohusu fani kwani hakuzungumzia upande wa msuko na matumizi ya lugha ambapo katika utafiti huu mtafiti alifanyia uchunguzi masuala hayo. Tafiti ya Traure (2002) ilisaidia sana kazi hii kwenye kubaini maudhui katika nyimbo husika za kazi hii na hata kubaini mapengo ambayo Traure hakuyaziba kwenye kazi yake.

Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), maudhui ni kile kinachozungumzwa kwenye kazi ya kifasihi. Ni mkusanyiko wa mambo yote kwa ujumla yanayoangaziwa ukiwemo msimamo wa mwandishi juu ya mambo au mawazo hayo. Anafafanua zaidi na kusema kwamba vipengele vya maudhui ni vingi vikiwemo dhamira, migogoro, na itikadi. Maelezo haya ya Ntarangwi yalitufaa sana katika kuhakiki maudhui ya nyimbo za msanii *Embarmbamba* kwenye vipengele vilivyotajwa hapo juu.

Mutwiri (2005), alihakiki nyimbo kulingana na utendakazi wake pale alipofanya utafiti wake akizingatia na kueleza umuhimu wa nyiso za Watigania. Utafiti wake ulitofautiana na huu kwani utafiti huu ulijikita katika uchambuzi wa kipengele cha mtindo kwa ujumla na wake ulizingatia utendakazi pekee. Ijapokuwa Mutwiri aliangazia upande tofauti kabisa na wa kazi hii, kazi yake ilibainisha wazi mapengo ambayo yamezibwa na kazi hii hasa kwenye kipengele cha kuangazia mtindo katika nyimbo husika za kazi hii.

Mwanza (2007), katika utafiti wake uliohusu mtindo wa nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Alijikita katika uteuzi wa tamathali za usemi katika nyimbo hizo husika. Utafiti huu utatufaa katika utafiti wetu kwani baadhi ya mambo aliyoyaangazia Mwanza yalifanyiwa utafiti kwenye mada yetu huku ikikumbukwa kwamba tamathali za usemi ni moja wapo ya mbinu za kimtindo kwenye kuziumba kazi za fasihi.

Katika utafiti unaohusu nyimbo za uganga wa pepo uliofanywa na Gora (2007), anatufahamisha jinsi lugha ilivyotumiwa kwa njia ya kisanii na kusheheni wingi wa matumizi kadhaa ya tamathali za semi. Utafiti wa Gora uliusaidia huu katika kuchunguza maudhui ya nyimbo za injili za msanii *Embarambamba*, ambazo bado hazijafanyiwa uchunguzi, sababu ambayo imefanya kuziba pengo lililoko la utafiti.

Katika utafiti unaohusu athari za nyimbo za harusi kwa mume na mke uliofanywa na Sayfa (2007), unasema kwamba nyimbo zinawajenga maharusi yaani mume na mke katika kustahimili ndoa na kuitunza ili idumu. Anasema kwamba jamii kwa ujumla hujengwa na maudhui katika nyimbo hizi, hasa katika kuikuza ndoa yenyewe na kuiweka wazi miiko yote katika maisha ya ndoa na hata kukifanya kizazi kitakacho kuja kuiendeleza tamaduni husika. Sayfa amejikita sana katika maudhui na kuangazia kwa uchache upande wa matumizi ya lugha, pengo ambalo limezibwa

Mount Kenya University

kwenye utafiti huu. Kazi ya Sayfa imeisaidia hii kwenye kuangazia maudhui yanayopatikana kwenye nyimbo za injili za Christopher Nyakwara Mosioma (*Embarambamba*).

Wamitila (2008), anaweka wazi dhana mbili zaa maudhui kwa kusema kwamba ni yale masuala ambayo mtunzi wa kazi ya kisanaa ameyaangazia katika kazi yake na pia kusema kwamba maudhui ni ile maana inayoletwa na matini ya kazi husika ya mtunzi. Maelezo haya ya Wamitila yalitufaa katika kubainisha maudhui katika nyimbo za msanii *Embarambamba* katika kujikita katika misingi hii aliyoielezea.

Mwaniki (2011), alifanyia utafiti nyimbo za kikikuyu alizozitohoa msanii anayejulikana kama Salim Junior. Utafiti wake huo uliangazia sana masuala ya matumizi ya lugha ambayo yalizua mabaliko katika shuhuli za utohozi wa nyimbo hizo. Utafiti wake Mwaniki uliangazia sehemu ya vipengele vya kimtindo jambo ambalo litatufaa kwa kiasi kikubwa kwenye utafiti huu. Kazi yake iliusaidia utafiti huu kwenye kuangazia matumizi ya lugha n ahata kubaini njia kadhaa za kimtindo ikiwemo utohozi ambayo ilibainika kwenye za zilizolemgwa na kazi hii.

Kwenye uhakiki wa uchocheaji wa mabadiliko kupitia nyimbo uliofanywa na Mbilikile (2014), anasema kuwa nyimbo zimetumika pakubwa kwenye kuleta mabadiliko yakiwemo ya maadili, tabia, mienendo na hata majukumu ya uamuzi katika shuhuli za kiuongozi. Mbikile ametueleza kwamba nyimbo za Bongo flavor zimeleta athari kubwa katika kuijenga na kuiadilisha jamii katika masuala tofauti tofauti. Utafiti huu wa Mbilikile ulinisaidia kuona jinsi ya nyimbo za Bongo Fleva zinavyo athiri jamii. Kazi ya Mbilikile ilifaa kazi hii kwenye kuangazia athari za matumizi ya lugha na maudhui ya nyimbo za msanii wa nyimbo za injili za Christopher Nyangwara Mosioma.

Utafiti mwingine wamchango wa nyimbo katika jamii ulifanywa na Mohamed (2014), alipohakiki mchango wa nyimbo za ngoma za kidatu katika jamii. Alisema kwamba nyimbo zina dhima tofauti

tofauti katika jamii zikiwemo zile za kuadilissha, kuasa, kukejelina hata kupataia mawaidha kuhusu ndoa na shuhuli zingine za kijamii. Mohamed anazidi kusema kwamba nyimbo zina athari na mchango mkubwa katika kuijenga jamii na kudumisha utamaduni na historia ya jamii husika. Kazi hio ilisaidia kazi hii kwa kiasi fulani kwa kuwa inaongelea mambo yanayoegemea maudhui ya nyimbo kwa kutathmini athari na hata kutaja uhusiano uliopo na athari zinazojitokeza.

Katika utafiti uliohakiki muingiliano wa tanzu tofauti tofauti za fasihi simulizi uliofanywa na Simiyu (2015), alithibitisha jinsi tanzu za fasihi simulizi zinavyoweza kuwa vijenzi vimoja katika mtungo mmoja. Alitafiti mambo haya akiangazia kazi za fasihi simulizi za kiafrika akiangazia Embalu na Mwaka Kongwa. Kazi ya Simiyu iliufaa utafiti huu kwa kiwango kikubwa mno hasa katika kuonyesha na kueleza maudhui katika utunzi wa msanii wa utafiti huu anayetafitiwa.

Yonazi (2021) katika utafiti wake kuhusu matumizi ya Usanaa wa lugha kwenye kuzijenga dhima za nyimbo za Waasu za harusi, alibainisha vijenzi kadhaa vinavyohusisha usanaa huu wa lugha ambapo mbinu za tashbihi, dhihaka na mbinu nyinginezo hutumiwa kwa kiasi kikubwa katika kuwasilisha dhima zilizolengwa kuwasilishwa na nyimbo hizo. Mbinu hizi huzua hisia inayokusudiwa kwa walengwa na kuupitisha ujumbe uliokusudiwa na njia mwafaka zaidi. Utafiti huu ulitufaa katika mada yetu ya kuangazia matumizi ya lugha katika mada yetu.

Aboge (2021) alipotafiti kuhusu matumizi ya usimulizi kama mtindo katika nyimbo za Bahati Bukuku alifafanua kwa mapana jinsi usimulizi unavyosaidia katika kuwasilisha maudhui katika nyimbo teule za mwimbaji huyo. Utafiti wa Aboge umetoa ufafanuzi wa dhana ya maudhui kwa kurejelea maoni ya wataalamu mbalimbali ambao wamechangia kuhusu dhana hii muhimu katika usimulizi. Vilevile amehakiki baadhi ya maudhui yanayopatikana katika nyimbo hizo teule, kwa mfano, Imani ya dini, Unafiki, Msamaha, Nafasi ya marafiki katika maisha ya mja, Ushirikina, Anasa na majukumu ya jinsia ya kike miongoni mwa wanajamii. Utafiti huu ulitufaa katika

kuangazia mtindo kwa kuegemea kazi za msanii lengwa wa kazi yetu na kubainisha maudhui kadha wa kadha katika nyimbo zake.

Tunaporejelea maadishi ya vitabu na makala ya tafiti mbalimbali zilizofanywa, ni dhahiri kuwa hakuna watafiti ambao wameshughulikia uhakiki wa mtindo aliyoutumia mwimbaji wa nyimbo za injili Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba)* katika kusuka maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo zake, pengo ambalo utafiti huu limetarajia kuliziba.

## 2.2 Misingi ya Nadharia

Kulingana na Wafula na Njogu (2007) wameelezea nadharia kama mawazo ambayo yamepewa makusudio ya kuangazia ufahamu wa kueleza ukweli wa shuhuli au tabia fulani. Kazi hii yetu iliongozwa na nadharia ya Simiotiki ambayo iliasisiwa kutokana na nadharia ya Umuundo ya Ferdnand Dessaussure (1960), na kuwekewa misingi na wataalamu tofauti tofauti miongoni mwao akiwa Noam Chomsky (1995).

Kulingana na Nazarova (1996), anafafanua simiotiki kama maalezo ya matumizi ya alama kwenye jukumu la kutumia lugha. Anaendela kueleza zaidi kwa kutilia mkazo kwamba sharti pawe na alama na kile kinachosimamiwa na alama husika huku kukitiliwa maanani sharti la kuwa alama hio iwe inakubalika na wanajamii.

Katika matumizi ya alama, Chandler (1992), anafafanua kuwa binadamu ni muumbaji wa alama na huziunda alama hizi kwa ubunifu mkubwa na kuzikusudia tafsiri inayoendana na alama husika. Wanaweza kufanya hivi kwa njia nyingi hata ikiwemo ile ya kutumia wanyama au hata vitu visivyokuwa na uhai kupewa sifa za binamu na hata kurejelea mienendo ya binamu ili kulifikia shabaha la kazi ya fasihi lililokusudiwa.

Mount Kenya University

Nadharia ya simiotiki inafafanua mihimili yake ikiegemea mfumo wa ishara na kuleta maana kutokana umbo au ishara iliyokusudiwa. Katika mhimili wa kwanza wa nadharia hii ni kwamba katika mawasiliano ya wanajamii ya kila siku sharti pawepo na matumizi ya ishara zinazokubaliwa na wanajamii kuashiria maana fulani inayoeleweka na wanajamaii wote. Ni katika matumizi ya ishara hizi za kinasibu ndipo maana inayokusudiwa huzinduka na kuleta mawasiliano ya moja kwa moja au hata ya kimafumbo. Mtafiti alitumia mhimili huu kwa kuelezea athari ya matumizi ya maneno katika kazi za msanii lengwa wa utafiti huu katika kuzua maudhui ya kazi zake kwa hadhira aliyoikusudia. Mtafiti alifahamu kwamba matumizi ya maneno nasibu ndio huzua ishara kwenye kurejelea dhana iliyolengwa na maneno yaliyotumiwa.

Katika kuelezea mhimili mwingine wa nadharia ya simiotiki ni ile dhana ya kitaja na kitajwa. Mhimili huu unaeleza kwamba hakuna uhusiano wa moja moja kati ya kitaja na kitajwa bali uhusiano huwa ni wa dhahania tu. Hali hii inaletwa na ukweli kwamba matumizi ya lugha huwa aghlabu ni ya kubuni tu na maana ya neno moja linaweza kubadilika kutoka kwa lugha moja hadi lugha nyingine. Lugha inapotumiwa huegemea zaidi katika taswira, matumizi ya picha na hata ishara ila pasiwe na maana ya moja kwa moja na kile kinachosemwa au hata kuandikwa (Ntarangwi 2004). Ni katika kuegemea mhimili huu ambapo mtafiti aliweza kuangazia kwa mapana mambo yafuatayo katika utafiti wake:

Katika kuelewa maana na lengo lilokusudiwa na mwandishi fulani ya kazi ya fasihi kulingana na Barthes (1994), anaeleza kwamba, ufahamu huo huegemea misimbo mitano ya Nadharia ya simiotiki. Misimbo hii anayoitaja Barthes ni Kiseme, Kiutamaduni, Kihemetki, Kimatukio na kiurejelezi. Waumbaji wengi wa kazi za fasihi wanaweza kuitumia misimbo hii kwenye ubunifu wao kwa kuwa na ufahamu nayo au hata kwa kutoifahamu kabisa. Katika kuichambua data ya utafiti huu, mtafiti alitumia misimbo yote hii mitano kwakufuata maelezo haya:

Kwenye maelezo ya Msimbo wa Kihemetiki ni ile maana inayojitokeza kutokana na anuani ya kazi fulani ya kifasihi. Ni kutokana na maneno yaliyotumiwa kuunda anuani ya kazi husika ya fasihi ambapo msomaji anaweza kupata moja wapo ya maudhui ya kazi hio. Hivyo basi msimbo huu ulimwezesha mtafiti kuweza kukamilisha lengo lake la kwanza la utafiti huu kwa kubainsha maudhui ya nyimbo za msanii Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba).*

Kwenye maelezo ya msimbo wa Kiseme ni kuwa maneno yote katika hali yake ya matumizi sharti yawe yanawasilisha maana kisemantiki kama anavyosema Mark (1995). Wapo watunzi ambao huteua maneno fulani kuwasilisha maana tofauti inayowasilishwa na maana ya maneno hayo kwa hali ya ukawaida. Katika nia ya kufanikisha lengo la pili la utafiti huu, mtafiti aliutumia msimbo huu kuchambua mtindo wa msuko wa maudhui na matumizi ya lugha yanayopatikana katika nyimbo teule.

Maelezo ya msimbo wa kiurejelezi kama Ntarangwi (2004), anavyotueleza, ni ile dhana ya kutumia sifa za kiumbe fulani kuelezea tabia ya kiumbe kingine kwa njia ya ufanisho wa moja kwa moja. Mara nyingi mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kumpa mwanadamu sifa za mnyama kama moja wapo ya mitindo katika kutilia mkazo maelezo ya tabia fulani ya wahusika wake kwenye utunzi wake. Katika kulifanikisha lengo letu la pili kuhusu kuchanganua matumizi ya lugha katika nyimbo za msanii husika na hata kubainisha maudhui yanayojitokeza kwayo, msimba huu ulitufaa sana.

Kwa kuelezea Msimbo wa kimatukio, ni ile dhana ya watunzi wa kazi za kifasihi kubuni matukio ya kiishara na kimsimbo katika kuzijenga kazi zao. Anaweza kubuni kisa ambacho watendaji wake nii wanyama ilhali kwa uhalisia vitendo vile vinaweza kufanikishwa tu na upekee wa uwezo wa kibinadamu. Msimbo huu ulituwezesha kuchunguza matukio yanayowasilishwa mbele yetu

kupitia nyimbo za msanii tulizozitafiti na tukaweza kupata msuko aliyoutumia na kubaini mtindo aliyouegemea msanii.

Mark (1995), anauelezea msimbo wa kiutamaduni kama dhana ya kutumia viashiria vya kiutamaduni katika kulijenga lengo la kazi ya fasihi. Viashiria hivi vya kiutamaduni vinaweza kuwa mavazi, chakula na vinginevyo kulingana na mila na tamaduni za jamii husika. Hivyo basi, tunapochambua nyimbo za Christopher Nyagwara Mosioma (*Embarambamba)* niliangazia kwa makini matumizi ya viashiria vya kiutamaduni katika nyimbo zake kwani ni katika viashiria hivyo ndipo tulipopata na kufahamu maudhui ya kazi za msanii husika na kuwezesha kuafikia lengo letu la tatu.

Kulingana na maelezo ya kina ya hapo juu, nadharia hii ilitufaa zaidi kwenye kuchambua data ya nyimbo za msanii Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarmbamba)* na kufanikisha malengo yetu ya utafiti.

## 2.3 Hitimisho

Sura hii imeeleza kwa mapana yaliyoandikwa kuhusu mada ambapo waandishi mbalimbali wakiwemo Wafula na Njogu, Chandler (1992), Ntarangui na Mark (1992) wametajwa ili kuonyesha kazi zilizopitiwa na ufaafu wake kwenye kazi hii. Sura hii pia ilitaja nadharia iliyotumika nayo ilikuwa nadharia ya simiotiki. Nadharia hii iliangaziwa na mihimili na misimbo ambayo imetumika kufanikisha kuchanganua data ya kazi hii. Katika kuboresha na kufanikisha kazi hii, mbinu za utafiti zimejadiliwa kwa kina katika sura ya tatu inayofuata.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii imeshughulikia vipengele ifuatavyo; muundo wa utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu na vifaa vya kukusanya data, uchambuzi na uwasilishaji wa data na kumalizia na maadili ya utafiti.

## 3.1 Muundo wa Utafiti

Kwa mijibu wa Kothari (2004), anafafanua muundo wa utafiti kama mikakati ya kujibu swali la utafiti kwa kutumia data za majaribio zilizokusanywa.

Utafiti huu uliongozwa na muundo wa uchunguzi wa kinathari ambapo matokea ya utafiti huu yaliandikwa kufuata muundo wa kimaelezo. Katika kuzingatia muundo huu, tunaeleza namna mtindo wa msuko wa maudhui na matumizi ya lugha unavyojitokeza katika nyimbo za msanii Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*) tukitilia maanani malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia iliyochaguliwa.

## 3.2 Sampuli na Usampulishaji

Kothari (2004), anafafanua sampuli kama idadi au sehemu ndogo ya idadi kubwa iliyochaguliwa kwa lengo la kufanikisha shuhuli fulani. Kwa kuzingatia maelezo haya, tunaweza kusema kuwa sampuli ni kiasi fulani cha watafitiwa kinacho chaguliwa miongoni mwa idadi kubwa.

Kutokana na maelezo ya Spata (2003), William (2011) na Bryaman (2004), Usampulishaji ni ile hatua ya kuteua kundi dogo la watu au vitu miongoni mwa kundi lengwa kubwa katika utafiti kwa lengo la kuliwakilisha kundi lote katika utafiti, hii ni kutokana na kuwa, kushirikisha watu wote hakuwezekani. Kikundi hiki kidogo huteuliwa ili kufanisha ukusanyaji wa data.

Kazi hii ni ya fasihi simulizi kipera cha nyimbo. Sampuli lengwa ni nyimbo za injili na ambapo sampuli mahususi ni nyimbo za injili zilizoimbwa na Christopher Nyangwara Mosioma

(*Embarambam*ba) miaka ya 2021-2023 iliyoteuliwa kwa njia ya uteuzi wa kimakusudi ili kupata nyimbo zitakazotumiwa kama data katika utafiti huu. Nyimbo za msanii huyu ziliteuliwa kutumiwa kwa utafiti huu kwa sababu ya kuzua sintofahamu kwa hadhira na kuchukuliwa kuleta hisia za nyimbo za kiulimwengu japokuwa mwimbaji mwenyewe anadai kuegemea nyimbo za injili. Nyimbo zote za Injili alizoimba msanii Christopher Nyangwara Mosioma katika miaka ya 2021-2023 ni nyimbo kumi na moja. Mtafiti aliteua sampuli ya kimaksudi ya nyimbo zote kumi na moja za Injili za msanii husika katika kipindi cha wakati kilichokusudiwa ili kufanikisha malengo ya utafiti. Nyimbo hizi kumi na moja ndizo zilizopatikana kwenye mtandao kwani msanii mwenyewe hutoa nyimbo moja moja baada ya kipindi kirefu cha ukimya. Uteuzi wa kipindi cha nyimbo hizi uliteuliwa kwa sababu ya kimya kilichosheheni kwenye kutoa nyimbo za msanii huyu baada ya marufuku ya nyimbo zake, hivyo basi kufikia wakati wa kufanya utafiti huu nyimbo zilizokuwa kwenye mtandao zilikuwa za kutoka mwaka wa 2021-2023.

### 3.3 Mbinu na Vifaa vya kukusanya Data

Hatua ya mwanzo ya ukusanyaji wa data ilihusu uchaguzi wa nyimbo zinazohitajika katika utafiti kati ya nyimbo zote alizorekodi msanii Christopher Nyagwara Mosioma (*Embarambamba*) katika mwaka 2021-2023. Nyimbo hizi zilipatikana mtandaoni na maktabani. Nyimbo hizi zilihakikiwa kwa kusikilizwa kwa makini kulingana na malengo ya utafiti huu. Baada ya kusikilizwa, ziligeuzwa na kuwekwa kimaandishi ili kupiga jeki shughuli nzima ya ukusanyaji wa data zilizohitajika. Mambo haya yote yalifanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Vile vile mtafiti alidurusu na kunakili matini yote iliyohusiana na nadharia iliyochaguliwa ya Simiotiki. Ukusanyaji wa data pia ulifanikishwa kwa kusoma tasnifu za awali zilizoandikwa kwa kutumia nadharia ya

Simiotiki, makala ya mtandaoni, pamoja na majarida. Mtafiti aliandika matini yote muhimu iliyomsaidia kwenye utafiti wake.

Utafiti huu ulihusisha njia moja kuu ya uchunguzi ambayo ni usikilizaji makini wa nyimbo husika. Nyimbo hizi ziliwezesha uteuzi wa vipengele vinavyotafitiwa kupata fursa ya kudondolewa na kuhifadhiwa kwa njia ya maandishi kwenye daftari maalum. Aidha, maandishi yaliyoandikwa yalimpa mtafiti mwangaza kuhusu uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti lengwa.

### 3.4 Uchambuzi na Uwasilishaji wa Data

Kothari (2013), anaeleza uchambuzi wa data kuwa ni shuhuli nzima za utaratibu wa kutumia mbinu za takwimu na kimantiki ili kufafanua na kufupisha data iliyokusanywa kwa namna itakayopiga jeki mchakato wa kujibu maswali husika ya utafiti.

Uchambuzi wa data hufanya mambo ya kutafsiri kuwa rahisi hususan data ya moja kwa moja au hata katika kuisoma data yenyewe kwa nia ya kupata ujuzi, (Bogdan na Biklen, 1992).

Mbinu za uchambuzi wa data ni nyingi lakini data za kazi hii zilichambuliwa kwa kuongozwa na malengo mahususi. Kwa sababu ya hivyo, vifungu mbalimbali vya data vilivyokusanywa kutoka mtandaoni na makitabani kuhusu mada vilichanganuliwa kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki.

Data iliyokusanywa kutoka katika nyimbo zilizochaguliwa ilipangwa kwa utaratibu wa malengo ya utafiti. Mtindo huu uliupa muonekano wa mpangilio ufaao na uliorahisisha kuhusisha data pamoja na malengo ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuongozwa na vipengele vifuatavyo;

(a) Maudhui yanayoibuka katika nyimbo teule.

(b) Mtindo wa matumizi ya lugha katika nyimbo teule.

(c) Athari za mtindo wa msuko wa maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo husika.

Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa mtindo wa kimaandishi wa aya na kubainisha jinsi maudhui, mtindo wa msuko wake na matumizi ya lugha na athari zake zinavyojitokeza katika nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*) 2021-2023.

Kutokana na maelezo haya, matumizi ya data za kiuthamano ndiyo yaliyotumika kuwasilisha matokeo ya utafiti huu. Kama alivyoeleza Gray (2007), kuwa data za kiuthamano zimesheni maelezo mengi yanayofafanua matukio. Na kwa mkondo huo huo, mtafiti alihakiki maudhui pamoja na kuonyesha namna ambavyo vipengele vya maudhui, mtindo wa msuko wa matumizi ya lugha na athari zake zilivyojitokeza katika nyimbo teule za utafiti.

## 3.5 Maadili ya Utafiti

Katika maadili na kaida za utafiti, mtafiti aliomba ruhusa ya kufanya utafiti na hata kulinda siri za habari aliyoikusanya ili kuufanya utafiti wake ufaulu. Vile vile alizingatia kanuni za kisayansi, haki za binadamu bila kusahau ushirikiano baina ya jamii na sayansi.

Kwa kuzingatia hayo, mtafiti alipata waraka wa kung'oa nanga kwa utafiti kutoka Chuo kikuu cha Mount Kenya na baadaye kupataa kibali cha kufanya utafiti kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Utafiti huu ulifanywa kwa njia ya uadilifu na uwazi ambapo data iliyovumbuliwa imekuwa ya ukweli na ya kuaminika na ambayo itaweza kuthibitishwa na watafiti wengine baadaye.

## 3.6 Hitimisho

Sehemu hii imeshughulikia mbinu za utafiti. Mambo yaliyoshughulikiwa ni muundo wa utafiti ambapo muundo wenyewe ni wa kimaelezo ukifuatwa na sampuli na usampulishaji, ukusanyaji, kuchambua na kuwasilisja data. Katika kuichanganua data, maelezo ya kinathari ndio yaliyoelezwa kutumika na sampuli ya utafiti huu ilihusisha nyimbo za injili za Christopher Nyakwara Mosioma (Embarambamba) katika miaka ya 2021-2023. Data iliyokusanywa ili chambuliwa kwa kuongozwa na vipengele vitatu.Mbinu iliyotumiwa kwa ukusanyaji data ilikuwa

ya usikilizaji makini wa nyimbo husika na kudondolewa mambo muhimu ya utafiti na kuwaandikwa ili kuhifadhi. Sehemu ya maadili yalihusisha zaidi kuweka siri ya data na kuomba kibali cha NACOSTI. Baada ya kuelezea mbinu za utafiti, sura inayofuata inahusu uchanganuzi wa data na ufasiri wa matokeo ya utafiti wenyewe.

Mount Kenya University

## SURA YA NNE

## UCHANGANUZI WA DATA NA UFASIRI WA MATOKEO YA UTAFITI

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia historia fupi ya maisha ya kibinafsi ya Christopher Nyangwara Mosioma (*Embaramababamba*) pamoja na kazi zake. Maelezo ya kina kuhusu Maudhui, Mtindo na Athari za matumizi ya lugha katika kazi za msanii husika pia yamejadiliwa.

### 4.1 Historia fupi ya Christopher Nyangwara Mosioma

Christopher Nyangwara Mosioma ambaye kwa jina la kisanii anajulikana kama Embarambamba alizaliwa tarehe moja mwezi wa Februari mwaka wa 1988 katika mji wa Keroka uliyoko kaunti ya Nyamira nchini Kenya. Ni baba wa watoto watano na mme wa mke mmoja aitwaye Phenny Osigei Nyangwara. Ni msanii ambaye historia yake ya elimu mpaka wakati wa utafiti wetu ilikuwa imekomea darasa la nane katika shule ya msingi ya Kierira DOK iliyoko katika eneo bunge la Kitutu Masaba. Kiu yake ya elimu iliishia hapo na kuanza shughuli za ukulima mdogo kabla ya kujitosa kwenye sanaa ya mziki baadaye.

### 4.2 Muhtasari wa Kazi za Mziki za Christopher Nyangwara Mosioma

Msanii huyu Christoper Nyangwara Mosioma alipachikwa jina lake la kisanii *Embarambamba* kutokana na ustadi wake wa upigaji ngoma, jina ambalo lilitokana na mfululizo wa mlio unatokana na weledi wa upigaji wa ngoma kwa njia ya madaha.

Katika shughuli za kuimba, aliweza kurekodi wimbo wake wa kwanza uitwao *Ensanako Tebwati Masikani* katika mwaka wa 2007 alipopewa usaidizi na rafiki yake wa ndani Bw. Ongengo. Msanii huyu kabla kuanza kuimba nyimbo za Injili alikuwa mwimbaji wa nyimbo za kiulimwengu ambapo aliweza kurekodi nyimbo kadhaa zikiwemo: *Amatingoro, Boda boda, Engiti, Nabo Ereigo, Transline Classic* na nyinginezo.

Baada ya miaka kadhaa badae aliamua kuegemea upande wa nyimbo za Injili ambapo alianza kutoa nyimbo zilizopendwa na kuangaliwa mno kwenye mitandao kwa sababu ya mtindo wake wa kucheza kwenye matope na juu ya mapaa ya nyumba.

Tasnifu hii imeangazia kwa kina nyimbo za Injili ambazo msanii huyu aliziimba kati ya mwaka ya 2021-2023 ambazo ni nyimbo takribani kumi na moja. Nazo ni: *Injili ni Tamu, Yesu Nimwagie, Imesimama, Nataka Nikuingize, Napenda Mbele, Ingia Ndani, God Is Good, Yesu Panua, Bend This way, Tuko Uchi* na *Yesu Ninyonye.*

### 4.3 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Katika kudukua nyimbo za Injili za msanii huyu baina ya mwaka wa 2021- 2023, ilibainika wazi kwamba nyimbo kumi na moja ndizo alizoimba na kuzipachika mtandaoni kwenye chaneli yake ya YouTube kwa jina "Embarambamba." Maelezo yanayofuata yanatokana na uchangunuzi wa data iliyokusanywa ili kuafikia malengo ya utafiti kama yalivyoangaziwa katika sura tatu.

### 4.4 Maudhui katika Nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambama*) katika Mwaka wa 2021-2023

Maudhui katika kazi ya fasihi ni mawazo yote kwa jumla ambayo msanii wa kazi ya fasihi amekusudia kuyaleta kwa hadhira. Ni katika maudhui ambapo anaweza kutoa msimamo wake au hata kuibua ujumbe alioulenga haswa kuuwasilisha. Kwa kawaida maudhui hujengwa na vipengele kadha wa kadha vikiwemo; falsafa, dhamira, msimamo, migogoro na hata ujumbe. Maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za injili za Christopher Nyakwara Mosioma katika miaka ya 2021-2023 ni kama yafuatayo:

#### 4.4.1 Maendeleo ya Kiuchumi

Kwa kawaida dhana ya uchumi hurejerelea mchakato mzima wa kuzalisha mali na hata njia za kuipata ili mja ajikimu kimaisha. Katika mhimili wa pili wa nadharia ya simiotiki unaotaja kitaja na kitajwa, mhimili huu unazungumzia kuhusu uhusiano uliopo wa kinasibu kwamba

kinachotajwa na kitaja hakina uhusiano wa moja kwa moja bali ni maana tu ya kinasibu inayopachikwa na watumiaji wa neno husika.Maneno yanayonasibishwa na hali za kiuchumi yanayopatikana katika nyimbo za msanii husika ni pamoja na: shida,viongozi, waliolala chini, kuwa ngambo, kupewa, kuishi vizuri, kuinuliwa, kukosa pesa na kupanuliwa kimaisha. Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma maudhui haya yanajitokeza katika nyimbo tano. Nazo ni; *Bend This Way, Napenda Mbele, Nataka Nikuingize*, *Nataka Kunyonywa* na *Yesu Panua*.

Msanii huyu kwenye wimbo wa *Bend This Way* anasema,

> *"......wengine walidharauliwa wako ngapi this way*
> *wengine walipitia shida wako ngambo this way*
> *waliodharauliwa leo  ni viongozi this way*
> *waliolala chini leo ni viongozi this way......"*

Katika maisha ya jamii kwa ukawaida, viongozi huchukuliwa kuwa watu wenye uwezo mkubwa kiuchumi na walio na ushawishi mkubwa katika kuzalisha mali katika jamii. Na kwa upande mwingine maskini katika jamii hudharauliwa na kuchukuliwa kupe ambao huwasumbua viongozi hasa katika kutaka kupata riziki zao za kila siku. Hapa ndipo haswa ambapo madharau anayozungumzia msanii huyu kwamba kuna wale waliodharauliwa, anamananisha kwamba wale waja maskini wasio na mbele wala nyuma waliodharauliwa sasa wamekuwa viongozi na hata kuhusishwa na kutegemewa kwenye mchakato mzima wa kuzalisha mali katika jamii. Ama kweli haya ndio maendeleo ya kiuchumi anayoyaongelea na kuyazua kwenye wimbo huu.

Ni kwenye wimbo uu huu wa *Bend This Way* anaposema,

*"....aombaye mwisho hupewa...."*

Katika maisha ya kila siku ya mja mwenye kipato cha chini daima hatosheki na kidogo anachopata, na kwa msingi huu hujikuta akiombaomba kwa wenzake na hata kuomba dua kwa Mola wake angaa siku moja amfungulie njia zake apate kipato cha kumtosheleza. Katika kupata kufanikiwa kwa kile alichoomba, bila shaka "kupewa" anakokuimba msanii huyu husika anamaanisha mja huyu kutoka kwenye kuombaomba na kuwa mtu aliye kwenye kiwango kingine cha kujitosheleza.

Maneno haya yanadhihirisha wazi maendeleo ya kiuchumi. Kwamba mtu anaweza kutoka kwa umaskini alikodharauliwa na kupanda ngazi kiuchumi hadi kuwa kiongozi, jambo ambalo ukiliomba kwa Mwenyezi Mungu linawezekana.

Kwenye  wimbo wa *Napenda Mbele*, msanii anaendelea kusema,

*".....ukitaka kuishi vizuri ni Simba wa Yuda...."*

Kuishi vizuri kwa mtazamo wa kiuchumi ni kumiliki kila unachotaka kwa uwezo wa mwenyezi Mungu. Mtu aishipo vizuri umaskini humuondokea. Ni katika kuishi vizuri ambapo mja huweza kuupiga teke umaskini na kutia kiywani anachotaka na wala si anachopata. Kuishi huku vizuri husheheni mlo wa mara kwa mara usiokosekana, majumba ya kifahri, magari, starehe za kutajika na hata mazingira ya kuishi yenye kufurahisha mwili na moyo.

Embarambamba anaendeleza maudhui haya kwenye wimbo uitwao *Nataka nikuingize* anaposema,

*"..........nikiwa ndani nitainuliwa juu............"*

Msanii huyu anaeleza mtazamo wa kumtegemea Mungu na hata kuwa ndani wa mwongozo wa Mwenyezi Mungu ambapo anasisitiza kwa sababu ya hali hio, mja lazima atainuliwa juu kiuchumi. Kuunuliwa huku juu, kunashirikisha kubadilika kwa kipato ambacho kinatolewa kutoka chini na kuwekwa kiwango cha juu. Matumaini haya ndio yanayomfanya msanii huyu kusisitiza kumtegema Mungu na kutaka kudumu ndani yake daima dawamu.

Kwenye wimbo wa *Nataka Kunyonywa* anazidi kusema maneno haya:

*"…………..naomba kunyonywa dhambi za kukosa pesa……………..."*

Ni wazi kwamba msanii huyu analeta maudhui ya maendeleo ya kiuchumi kwani katika shuhuli zetu za kila siku, kila mja hujishirikisha kusaka hela angalau kujikwamua kutoka kwenye matatizo yake. Ni katika kupata pesa ambapo mtu huwa na uwezo mkubwa wa kujiendeleza kiuchumu na kujijenga kwa mtazamo wa kuwa tajiri.

Tunapomalizia kwa maneno ya wimbo uitwao *Yesu Panua* anazidi kusema,

*"………….Yesu panua maisha yangu…………..."*

Tukijikita kwenye dhana ya kupanuliwa kimaisha tunarejela hali ya kuwa na kila kitu unachokitaka na hata kumiliki mali na mambo yote ya ukwasi. Ni katika kupanuliwa huku kimaisha ambako msanii huyu anaomba kufanyiwa na Mungu ili azidi kuona faida ya kuwa katika maisha ya uokole.

### 4.4.2 Ulokole

Dhana ya maisha ya kilokole hurejelea maisha ya mtu ya kiungu ambayo huhusisha matendo ya kitakatifu yaliyosheheni kumtukuza na kumuenzi Mwenyezi Mungu kwa kila upande. Dhana ya mambo ya kiulokole yameelezwa zaidi na mhimili wa pili wa nadharia ya simiotiki. Mhimili huu

una misimbo mitano kama nilivyoelezea hapo awali. Msimbo mmoja ni Kiutamaduni unaorejelea mambo yanayozungumziwa katika kazi ya kisanii ambayo hurejelea matendo ya kitamaduni ya jamii fulani. Utamaduni huu unaweza kudhihirishwa kwa njia ya chakula, mavazi, mienendo ya kila siku na hata utaratibu wa kutenda mambo. Ulokole ni moja wapo wa tamaduni za wanaoamini utakatifu wa Mungu na hata kutaka kuudumisha kwenye maisha yao ya kila siku. Dhana ya ulokole imejidhihirisha wazi kwenye nyimbo za msanii huyu husika kwa kuwepo kwa maneno kama: kwa Mungu, pea Mungu maisha yako, kupata baraka, kuokoka, kumuimbia Mungu na kunyonywa dhambi. Maudhui ya ulokole katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma yanajitokeza katika nyimbo zifuatazo:

Kwenye wimbo wa *Ingia Ndani* alioimba na msanii Cyrus Koech anasema,

*"......ingia ndani......kwa Mungu huezi fukuzwa..."*

Maneno haya yanaashiria mwanzo wa mtu aliyefika mwisho katika matumaini, msanii huyu anamsihi mtu huyu kuanza maisha ya uongofu kwani kila mtu anakaribishwa bila kuangaliwa mienendo ya maisha yake ya awali.

Christopher anaendeleza maudhui haya pia katika wimbo wake wa *Imesimama* anaposema,

*".....pea Mungu maisha yako..........ya dunia yatapita....."*

Maneno haya yanadhamiria kumshauri mwanadamu kuacha maisha yake ya dhambi na kuanza maisha matakatifu kwani duniani sisi sote ni wa pita njia.

*".......tunapata baraka tukiwa ndani...."*

Haya ni maneno yanayopatikana kwenye wimbo uitwao *Nataka Nikuingize* yakiashiria mtu anapokuwa kwenye maisha ya kilokole basi hana buni kubarikiwa kwani ndivyo yalivyo maisha ya kiungu.

Katika wimbo wa *God Is Good* msanii anaendeleza maudhui ya ulokole anaposema,

> *".....kama umeokoka kaa kama number plate ya gari..."*

Kwa kusema hivi anarejela maisha ya uongofu kwamba mtu anapoishi maisha matakatifu matendo yake hudhihirisha wazi ukuu wa Mungu kama nambari za usajili zitambulishavyo magari. Anaendeleza zaidi maudhui haya kwenye wimbo uo huo anapozidi kuimba maneno haya,

> "*.....for the rest of my life I will sing for you*...." (kwa maisha yangu yote nitakuimbia).

Hapa anajaribu kusisitiza kwamba kwenye maisha ya kiongofu hakuna suala lingine la kufanya ila kumsifu Mungu kwa hali zote na bila kuwa na kikomo kivyovyote.

Tukiangazia maneno aliyoyatumia katika wimbo wa *Nataka Kunyonywa*, kwa mfano,

> *"....nataka kunyonywa dhambi zangu..."*

Hapa maudhui ya maisha ya ulokole yanajitokeza wazi kwamba ndio mtu aweze kuingia kwa uongofu sharti aombe msamaha kwa Mwenyezi Mungu ili asemehewe dhambi zake na kuanza maisha mapya ya uungu. Ikumbukwe kwamba hakuna mja asiyekuwa na dhambi ila jambo la msingi katika amaisha ya kilokole ni kutubu na kumpa Yesu maisha yako kwani ndiye anayetusamehe dhambi hizo na hata "kuziosha" dhambi hizo kwa damu iliyomwagika msalabani. Hivi ndivyo wanavyoamini wakristo.

### 4.4.3 Imani ya Kidini

Dini na Imani ni mambo mawili yanayoendana moja moja. Kama mhimili wa pili wa nadharia ya simiotiki unayvojieleza katika msimbo wa kiutamaduni ambao umerejelea matukio ya kijamii. Yapo matendo ya kijamii ambayo hudhihirisha imani ya kidini. Imani hii ya kidini ni moja wapo ya mambo ya kiutamaduni katika maisha ya binadamu ya kila siku. Maneno yanayopatikana kwenye nyimbo husika za utafiki huu yanayodhihirisha imani za kidini ni pamoja na:baba tukumbuke, uzima wa milele, nyumba ya Mungu, Yesu nimwagie baraka na Mungu ni kila kitu. Msimbo mwingine unaopatikana kwenye mhimili huu wa kitaja na kitajwa ni msimbo wa kimatukio. Kimatukio ni msimbo unarejelea matukio ya kiishara amabayo yanapatikana kwenye visa vinavyosimuliwa kwenye kazi za kifasihi. Katika nyimbo za kidini, mara  nyingi visa kutoka kwa vitabu vitakatifu husika hunukuliwa ili kuleta mafunzo na imani ya kidini katika kufanikiwa kwa matarajio ya waumini. Visa na matukio haya yanaweza kuwa matendo ya mitume na miujiza yao na hata hadithi zilizosimuliwa kwenye vitabu hivyo vitakatiifu vya dini. Maneno yanayodhihirisha haya katika nyimbo za Christopher Nyakwara Mosioma ni pamoja na: kama Abrahama na Sara na Daudi mchunga kondoo, ambayo ni maneno yanayohusiana na hadithi nilizosimulia hapo chini vyema. Dini ni Imani anayokuwa nayo mtu ikimhusisha Mungu au miungu juu ya maisha yake na hatima ya maisha hayo. Imani ya kidini ni kuamini mafunzo yanayohusiana na dini fulani.

Maneno yanayodhihirisha Imani ya kidini yanapatikana katika nyimbo zifuatazo:

Katika wimbo unaoitwa *Bend This Way* anatumia maneno haya

*"....baba tukumbuke na utubariki kama Abraham na Sara...."*

Kama wakristo wanavyomuita Abraham " baba wa imani" kwa kuangazia hadithi yake na mkewe katika kitabu cha Biblia cha Mwanzo kuanzia kifungu cha kumi na mbili. Ambapo Abraham na mkewew Sara wanafanikiwa kupata mtoto wakiwa wakongwe mno. Abrahama akiwa na miaka mia moja na Sara akiwa na miaka tisini wanatukiwa mtoto na mwenyezi Mungu na kumuita Isaka. Ni kutokana na hadithi hii ya Abraham ambapo msanii huyu anakuwa na imani ya kumtumainia Mungu na kuamini kwamba hata kama matamanio yake yatakawia ipo siku yatatimia kama vile mbavyo Sara na Abraham walivyopata mtoto wakiwa wazee mno.

Ni katika wimbo uu huu pia, anapoendeleza maudhui haya zaidi anaponukuu matukio ya hadithi ya Daudi mchunga kondo kwenye Biblia kwenye kitabu cha Samuel,mlango wa kumi na saba kuanzia mstari wa kumi na tano. Hadithi hii inahusisha matukio ya Daudi ambaye alikuwa kijana mdogo sana katika familia ya Yesse. Hadithi ya Daudi mchunga kondoo inahusisha matukio ya kivita ambapo kijana huyu alimuua mfilisti mmoja ambaye alikuwa anaitwa Goliathi. Mfilisti huyu alikuwa jitu la miraba minne na ambaye alikuwa amejihami kwa upanga, ngao, mkuki na mishale ilhali Daudi alikuwa na kombeo tu kuapa kuamini nguvu za Mungu wake wa Israeli. Imani aliyokuwa nayo Daudi alimpiga Goliathi jiwe moja tu kichwani nakumuangusha kifudifudi na kuuchukua ushindi wa vita vile. Ni katika imani hii juu ya Mungu wa Israeli inayomplelekea msanii huyu husika kuamini kwamba tumaini lake kwa Mungu si la kubahatisha.

Maudhui haya yanaendelezwa zaidi katika wiimbo aliyouita "*Nataka Nikuingize"* anaposema

> *"....kwa Yesu kuna uzima wa milele..."*

Ni katika kujikita katika imani ya dini yake Christopher Nyangwara Mosioma ambapo matumaini yake ya mzima bila kuwa na udhaifu wowote miaka na mikaka anayaweka.

Matumaini haya anayaweka katika kuamini uongofu ambao utamwezesha kufika "mbinguni" kusipokuwepo na taabu wala njaa.

Maudhui haya pia yanajitokeza kwenye wimbo ujilikanao kwa jina "*God Is Good* " anaposema

*"....nyumba ya Mungu iko na furaha tele...."*

Nyumba hii anayoirejelea msanii huyu kwenye wimbo wake huu anarejelea "makao ya milele" amabayo wakristo wanaamini kwamba mwongofu anapofariki huenda kuishi kwa "Baba" (Mungu). Ni katika makao haya ambapo daima kuna kuimba na kusifu, asali na maziwa kwa wingi, furaha anayoitaja msanii Christopher Nyangwara Mosioma.

Kwenye wimbo aliyoupa jina la "*Yesu Nimwagie"* aliyaimba maneno haya

*"...Yesu nimwagie uzima wa milele na baraka...."*

Katika imani ya kikristo wanaamini kwamba kila kitu hutokana na kudra ya mwenyezi Mungu. Kila wanaposali wanaiweka imani ya kujibiwa maombi yao kwa "Mwana wa Mungu" (Yesu) ambaye kupitia yeye maombi yao hujibiwa na Mwenyezi Mungu. Ni katika imani hii ambapo msanii huyu anamuomba Yesu amumwagie uzima na baraka daima dawamu bila kukoma.

Nikihitimisha kuangazia maudhui haya namalizia kwa kuujadili wimbo unaoitwa "*Nataka Kunyonywa"* pale ambapo Embarambamba alitumia maneno haya

*".....Mungu ni kila kitu..."*

Katika kujikita katika imani ya dini ya kikristo, kila litokealo katika ulimwengu huu limepangwa na Mwenyezi Mungu. Iwapo Mungu hataki hajapendezwa na jambo kutokea basi jambo hilo

haliwezi kutokea kamwe. Ni katika matumaini haya ambapo Christpher Nyangwara Msioma anasisitiza kwamba Mungu ni kila kitu katika maisha yake.

### 4.4.4 Ukuu wa Mungu

Ukuu wa Mungu ni maudhui ambayo hujitokeza kwa kiwango kikubwa katika nyimbo za kidini. Katika msimbo wa mhimili wa pili wa kitaja na kitajwa, kuna msimbo wa kimatukio ambao hurejelea matukio ya kiishara ambapo matukio haya husheheni matendo na visa. Visa hivi huangaziwa kwenye kazi za kisanii ili kuleta mafunzo na kuzungumzia mambo yanayopatikana katika jamii. Visa hivi pia husheheni tamaduni na mila zinazopatikana katika jamii husika. Mila na tamaduni zinahushwa na msimbo wa kiutamaduni ambao huegemea viashiria vya kitamaduni vinavyopatikana kwenye utunzi wa kazi za fasihi. Matendo makuu ya Mungu yanadhihirisha wazi tamaduni hizi na kuzua ukuu na uwezo aliyonao Mwenyezi Mungu. Maneno yaliyotajwa kwenye nyimbo husika yanayo dhihirisha tamaduni hii ya kiimani ni pamoja na: baba uliyeumba, nyumba ya Mungu iko na makao mengi, ndege kusifu Mungu, Mungu kufahamu maovu yetu yote, baba wa mbinguni, mkate na maji ya uzima, Mungu ni kila kitu, Dunia ni ya Mungu na Mungu kuimba mbingu na nchi. Dhana hii husheni sifa na mambo ambayo hupewa Mwenyezi Mungu kuelezea uwezo alionao ambao mwanadamu wa kawaida hawezi kuufikia hata chembe. Asilimia kubwa ya nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma zinadhihirisha maudhui haya, nazo ni kama zifuatazo:

Katika wimbo uitwao *Bend This Way* msanii anaanza kwa kuimba maneno haya;

> *"......baba mwenye uliniumba..."*

Kauli hii inaonyesha Mungu pekee ndiye aliyeumba kila kitu duniani na ni yeye pekee ndiye aliye na uwezo huo. Anwani ya wimbo huu pia inaashiria miondoko ya kuonesha ukuu wa

Mungu. Unapotaka kuonyesha ishara ya kuonyesha heshima kwa mtu unamuinamia (*bend*) kuonesha heshima na ukuu aliyonao. Ikumbukwe kwamba sheria moja wapo ya zile sheria kumi za Mungu katika kitabu kitakatifu cha Biblia cha Kutoka mlango wa Ishirini, mstari wa kwanza hadi wa tano, ina sema;

> *"Mungu akanena maneno haya yote akasema,Mimi ni Bwana, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini dunianii, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; ......."*
>
> ***Kutoka 20:1-5***

Ni katika sheria hizo kumi ambazo wakristo wanaamini kwamba kwazo wakizifuata basi watauona ufalme wa Mungu na kuamini kwamba Mungu peke ndiye wakuabudiwa.

Maneno yaliyokwenye wimbo uitwao *God Is Good* yanaashiria ukuu huo wa Mungu, pale msanii huyu husika alipoimba;

> *"......nyumba ya Mungu iko na makao mengi......"*

Ukuu huu wa Mungu unarejelewa na kuwepo kwa makao mengi ambayao kulingana na imani ya kikristo unaweza kumhifadhi kila mja ambaye amemtii na kufuata mafundisho ya dini hio.

Maudhui ya Ukuu huu wa Mungu yanaendelea kujadiliwa na kupewa sifa za kuimbwa hata na ndege, ambapo msanii huyu katika wimbo aliyouita "*Tuko Uchi*"anasema;

> *"....kama ndege wanakusifu wacha mimi nikusufu kila wakati......Mungu apewe sifa milele na milele........Mungu unainua mpaka wanyonge....."*

Sifa hii ya Ukuu wa Mungu anaiendeleza hata katika kujua maovu yote tunayoyafanya kwa kisiri, kwamba Mungu anayajua yote anapoimba kwa kusema

*"........maovu yote tuyafanyayo anayafahamu kwani tuko uchi mbele zake....."*

Mambo yote yanayotendeka duniani hutendeka kwa mapenzi ya Mungu na kwamba hakuna ambalo litafanyika kama Mungu hajaridhia. Kauli hii inadhihirika wazi katika maneno ya wimbo wa *Yesu Nimwagie* anaposema;

*"......Baba yetu wa mbinguni, mapenzi yako yatimie....."*

Maneno haya yanalandana sawasawa na methali inayosema *jitihada haiondoi kudura*, kwani kila tufanyalo hutegemea mapendeleo ya Mwenyezi Mungu ili kufanyika. Ni wazi kwamba mbele za Mungu viumbe vyote vilivyopo chini ya jua ni dhaifu na kamwe haviwezi kushindana na Mwenyezi Mungu.

Anaendeleza ukuu huu wa Mungu hata katika kupata riziki na kunyesha kwa mvua anapoimba maneno haya kwenye wimbo uo huo wa *Yesu Nimwagie*;

*"........ukiwa kwa maji wewe ni maji ya uzima........ukiwa kwa chakula wewe ni mkate wa uzima...."*

Maneno haya yanadhihirisha kwamba ukiwa wakumtegemea Mungu basi kila kitu chako kitafaulu kwani yeye pekee ndiye mtoa riziki. Katika kutathmini maneno haya ni wazi kwamba hakuna binadamu aliye na uwezo wa kumfungia binadamu mwingine kupata riziki. Uwezo huu ni wa Mungu pekee na katu hawezi kumnyima mja wake mkate wa kila hata kama kiduchu. Ikumbukwe kwamba kauli inaendana sawa na maneno yaliyoko kwenye sala moja ya wakristo ujulikanayo kama sala ya Bwana inayopatikana kwenye Biblia takatifu kwenye kitabu cha Mathayo, mlango wa sita, mstari wa tisa hadi ule wa kumi na tatu, inayosema;

*" Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliyembinguni, jina lako litukuzwe, Ufalme wako na uje,mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu, utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni,*



Mount Kenya University

*lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu na utukufu, hata milele. Amina.''*

***Mathayo 6:9-13***

Msanii huyu Christopher Nyangwara Mosioma anaendeleza maudhui ya ukuu wa Mungu hata kwenye uwezo wa kipekee wa kusamehe dhamabi za binadamu, kama alivyoimba kwenye wimbo aliyouita *Nataka Kunyonywa* anaposema;

*"......Mungu ni kila kitu atakunyonya dhambi zote...."*

Katika maisha ya kikristo ya kila siku, kutubu dhambi ni jambo la msingi katika kudumisha utakatifu wa maisha ya uongofu. Imani hii inatokana na matumaini kwamba Mungu ni mwenye huruma na ndiye pekee mwenye uwezo wa kutusamehe dhambi zetu pindi tunapomuomba msamaha.

Ukuu wa Mwenyezi Mungu unaendelea kujengewa misingi katika wimbo wa *Yesu Panua* alipoimba maneno haya;

*"...........hii dunia ni ya Mungu......ukicheza na neno la Mungu litakugonga........"*

Katika mafundisho ya dini ya kikristo inaelezwa wazi kwamba Mungu ndiye muumba wa vitu vyote duniani na ni yeye pekee wa kuabudiwa. Msukumo huu ndio uliomfanya Christopher Nyangwara Mosioma kuyatumia maneno haya kwenye wimbo wake. Kama Biblia takatifu inavyosema katika kitabu cha Mwanzo, sura ya kwanza, mstari wa kwanza, inasema;

*"..........Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi."*

***Mwanzo 1:1***

Ni wazi kwamba Mungu pekee ndiye mmiliki wa dunia hii tunayoishi na huezi kupingana na neneo lake. Ukuu wa Mungu unaendelezwa kwenye uwezo wa hata kutopinga maneno yake kwani mwishowe utajipata umeumia kwa kuyakaidi.

### 4.5 Mtindo wa Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma (*Embarambamba*) katika Mwaka wa 2021-2023

Senkoro (1982) alifasiri dhana ya mtindo kwenye kazi ya fasihi kama njia ambayo msanii huiunda kazi yake na kuipa sura ambayo katika mtazamo wa kifani na kimaudhui hudhihirisha masharti au kaida zinazopaswa kufuatwa ama ni za upekee. Anaendeleza maelezo ya mtindo akisema kuwa ni mpangilio wa fani na maudhui yanayopatikana katika kazi fulani ya fasihi kwa namna ambayo hubainisha ama kuchipuza nafsi na hata upekee wa mtunzi wa kazi hiyo.

Kwa kuangazia fasiri hii hatuna budi ila kuelewa anachokifafanua gwiji huyu kwa mtazamo wa kuegemea kwamba mtindo hujumuisha mpangilio wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi ikichukuliwa kwamba mpangilio huu hujikita kwenye upekee wa msanii kwenye kazi yake husika. Ikumbukwe kwamba suala moja laweza kushuhulikiwa na mtunzi zaidi ya mmoja ila kwa jinsi ilivyowasilishwa likawa tofauti kabsa, jambo linalosababishwa na upekee wa kila mmoja.

Kwa upande wake Wamitila (2003) anafafanua mtindo kama ujumla wa mbinu au sifa za upekee zinazompa uwezo msanii kuufikisha ujumbe wake kwa hadhira na huangazia uwezo wa mwandishi wa kuunda kazi hio. Anafafanua zaidi kwa kuongezea kwamba, dhana ya mtindo ni zile sifa fulani mahususi za msanii au mazoea ya msanii husika zinazojidhihirisha katika fani yake, uzoefu wa msanii kwa maandishi yake, uteuzi wa maneno, tamathali za semi, kuakifisha, sentensi na mengineo, ni mambo yanayomtofautisha mwandishi mmoja na mwingine.

Jambo wanaloliangazia Senkoro na Wamitila ni moja, kwani wazi wanaangazia upekee wa msanii ijapokuwa Wamitila kaongezea jambo moja zaidi, ambalo linahusu namna ya mwandishi kuwa na uzoefu wa kubuni kazi zake kwa njia ambayo inadhihirisha upekee aliyonao. Tunapojikita kwa maneno haya ya Wamitila ni wazi kwamba tukiangazia mtindo wa msanii sharti kuwe na kazi kadhaa za msanii husika ndipo kubainike hali hii ya mazoea kwani ndio msingi haswa wa mtindo.

Ni kweli kwamba huwezi kubaini mtindo anaoutumia msanii fulani kwa kuangalia kazi moja tu yake au anayohusishwa nayo. Ni wazi kwamba mtindo huweza kubainishwa baada ya kuhakiki kazi nyingi za msanii husika na kufahamu hali fulani ya uzoefu wake kwenye kazi hizo.

Mtindo katika kazi ya fasihi kwa ujumla ni zile mbinu za kisanaa ambazo mtunzi wa kazi husika huzitumia katika kuuwasilisha ujumbe kwenye hadhira lengwa. Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma mitindo ifuatayo imedhihirika wazi:

**4.5.1 Takriri**

Hii ni mbinu ya urudiaji silabi, neno au hata fungu zima la maneno katika kazi ya fasihi. Mbinu hii hutumiwa ili kutilia mkazo ujumbe unaopitishwa katika kazi husika. Kama walivyoeleza Kahigi na mwenzake Mugyabuso (1979) kwamba takriri ni aina mojawapo ya usemi unaohusisha usemaji wa kurudiarudia maneno yayo kwa yayo kwa kimakusudi ili kutilia mkazo au kwa nia ya kusisitiza wazo fulani. Wanaendeleza fasili yao hii ya takriri kama urudiajirudiaji wa neno, kirai, sentensi, sauti au hata wa sauti katika utungo fulani wa fasihi.

Msanii huyu Christopher Nyangwara Mosioma amaeitumia mbinu hii ili kutulia msisitizo katika maudhui yanyimbo zake na kuleta mvuto kwenye uimbaji wa nyimbo zakke kwa hadhira.Takriri

katika nyimbo za injili za msanii Embarambamba imejitokeza katika nyimbo zake zote kama nilivyoangazia katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 4.1: Maneno Yaliyotakririwa

| **Anwani ya wimbo** | **Maneno yaliyotakririwa.** |
|---|---|
| *Injili ni Tamu.* | *"Injili ya Mungu ni tamu."* |
| *Yesu Nimwagie* | *"Yesu Nimwagie."* |
| *Imesimama.* | *"Imesimama" na "Injili itasimama."* |
| *Nataka Nikuingize.* | *"Nataka nikuingize ndani."* |
| *Napenda Mbele.* | *"Ninapenda mbele sitaki nyuma" na "Simba wa yuda."* |
| *Ingia Ndani.* | *"Ingia ndani" na "Kwanini."* |
| *God Is Good.* | *"God is good all the time" na "Nyumba ya Mungu."* |
| *Yesu Panua.* | *"Nasikia nikugonge" na "Panua."* |
| *Bend This Way.* | *"Bend this way."* |
| *Tuko Uchi.* | *"Kama ndege wanakusifu," "Baba nimeona nikusifu kila wakati" na "Tuko uchi."* |
| *Yesu Ninyonye* | *"Nataka kunyonywa dhambi zangu."* |

Katika wimbo wa *Injili ni Tamu* amerudia rudia maneno kama "*Injili ya Mungu ni tamu*" ili kuelezea jinsi maisha ya uongofu yalivyo na furaha tele. Ikumbukwe kwamba maudhui yanayohusiishwa na wimbo huu ni kuieneza injili na kuyasifia maisha ya uongofu. Katika kuyakariri maneno haya niliyoyaangazia hapo juu analeta msisitizo wa maudhui lengwa na kuweka bayana alichotarajia kufikisha kwa hadhira yake.

Katika wimbo aliyouita *Yesu Nimwagie* anarudia rudia maneno yanayosema "*Yesu nimwagie*" kuonyesha jinsi ukuu wa Mungu ulivyojaa baraka tele, uwezo ambao unaleta dhana ya wingi wa kitu kwamba Mungu anapokupa baraka, hakupi kwa ukawaida bali hukumiminia. Anachosisita hapa kutumia mbinu hii ni kwamba ukuu wa Mungu si wa kubahatisha na kwamba Mungu si mchoyo wa baraka zake.

Anarudia rudia maneno kama "*imesimama*" na " *Injili itasimama"* kwenye wimbo aliyouita "*Imesimama"* ili kuyakuza maudhui ya ukuu wa Mungu. Akielezea kwamba hakuna wa kulipinga neno lake na kutilia mkazo msimamo wa maamuzi ya Mungu usiyoweza kubadilishwa ila Mungu mwenyewe kupenda.

Kwenye wimbo wake kwa jina " *Nataka Nikuingize"* amekariri maneno kama "*nataka nikuingize ndani*" kutilia msisitizo wa maudhui ya kueneza injili na maisha ya ulokole. Wimbo huu unalenga kuwahubiria watu njinsi ya kuwaingiza waumini ndani ya maisha ya uongofu huku ukielezea faida ya maisha hayo yasiyo na mateso.

Baadhi ya maneno kama "*ninapenda mbele sitaki nyuma*" na " *simba wa Yuda*" yamerudiwa rudiwa kwa kiwango kikubwa katika wimbo aliouita " *Napenda Mbele*," hili ni kwa kusudi la kutilia mkazo maudhui ya maendeleo ya kiuchumi, ambapo anasisitiza kwamba mtu anapokuwa na maisha kiungu basi hali yake ya kiuchumi huimarika na kuwa maisha ya hali ya juu. Anaendeleza kusisitiza na kutilia mkazo maudhui ya ukuu wa Mungu pale anaporudia rudia maneno "*simba wa yuda"* akirejela ujasiri alionao Mungu na kwamba yeye ndio mmiliki wa dunia nzima anayoirejelea kama "yuda."

Maneno kama "*ingia ndani*" na "*kwanini"* yamerudiwa rudiwa kwenye wimbo uitwao "*Ingia Ndani"* ili kusisitiza wale wasiokuwa kwenye uongofu kuokoka na kuacha maisha yao ya

dhambi na kujiunga na waliomwamini Mungu. Anawashnagaa wale ambao wanaishi katika maisha ya dhambi kuwauliza “kwa nini” wanachelewa kumpa maisha yao Yesu, jambo linalo tilia mkazo maudhui ya kueneza Injili katika wimbo huu.

Anaendeleza kusisitiza maudhui ya ukuu wa Mungu kwenye wimbo aliyouita “*God Is Good*” alipoyarudia rudia maneno kama “*god is good all the time*” na *“ na nyumba ya Mungu*.” Urudiaji rudiaji huu wa maneno haya yanampa msikilizaji fursa ya kuelewa uwezo wa Mungu kwenye maisha yetu na mamlaka aliyonayo kwenye mafanikio yetu.

Anaporudia rudia neno “*panua*” kwenye wimbo kwa jina “*Yesu Panua”* anasisitiza maudhui ya maendeleo ya kiuchumi kwani anamlilia Mungu ayapanue maisha yake kiuchumi jambo analolisisitiza kwenye kiitikiocha huu. Anaifanya hadhira yake kupata ujumbe huu kwa uwazi na kuwapa sababu zakumtegemea Mungu kiuchumi.

Katika wimbo aliouita “Bend This Way” anayakariri maneno “bed this way” kutilia mkazo maudhui ya ukuu wa Mungu kwamba ukitaka kufanikiwa sharti umtii na kumuabudu (bend) Mugu pekee. Jambo alilolikariri kwenye wimbo mzima.

Anayaendeleza na kuyasisitiza maudhui ya ukuu wa Mungu kwenye wimbo wenye anwani “Tupo Uchi” anayarudia rudia maneno “tupo uchi” na “ndege wanakusifu.” Urudiaji wa maneno haya yanadhihirisha wazi uwezo wa kipekee wa Mungu ambao unaweza kuyabainisha maovu yote tunayafanyayo sirini na kwamba anaujua wote kwa tupo “uchi” mbele zake. Sifa na ukuu huu anausisitiza na kuupa sifa wa kuimbwa hata na ndege.

Uwezo na ukuu huu anaendelea kuutilia mkazo anaporudia rudia maneno “nataka kunyonywa dhambi zangu” kwenye wimbo “ Nataka Kunyonywa.” Urudiaji huu unamuweka msikilizaji wa

wimbo kwenye kina cha kueleza mamlaka aliyonayo mwenyezi Mungu kwenye hata kutusamehe maovu yetu tuliyoyafanya.

### 4.5.2 Kuhamisha Msimbo

Mtindo huu hujitokeza pale mtunzi wa kazi ya fasihi anapotumia lugha zaidi ya moja katika kuuwasilisha ujumbe wake. Lugha hizi hutumia sentensi kamili zinajitegemea katika kuleta maana katika kazi husika wala si neno moja moja kibahati nasibu. Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma mtindo huu umejitokeza kwenye nyimbo zifuatazo:

Jedwali 4.2: Maneno yaliyohamishiwa Msimbo

| **Anwani ya wimbo** | **Msimbo uliohamishwa** | **Tafsiri yake.** |
|---|---|---|
| *Injili Ni Tamu* | *"...eyero ero ingwansere" (Ekugusi)* | "Hii nayo ni tamu." |
| | *"Dance like a snake" (Kimombo)* | "Cheza kama nyoka." |
| *Imesimama* | *"...gaki ningeeteneine."* | "kweli imesimama." |
| | *"...bono iga ningeeteneine."* | "sasa hivi imesimama." |
| | *"Barogi mbakonyetangaa."* | "wachawi hawawezi isimamisha." |
| | *"...abaibi mbako nyetanga." (Ekigusii.)* | "wezi hawawezi isimamisha." |
| *Ingia Ndani.* | *"our Redeemer is the King of universe." (Kimombo.)* | "Mhuishi wetu ni faMlme wa ulimwengu." |
| *God Is Good.* | *"God is good all the time." (Kimombo)* | " Mungu ni mwema kila wakati." |
| *Bend This Way.* | *"bend this way." (Kimombo)* | "inama hivi." |

Mount Kenya University

Christopher Nyangwara Mosioma ameitumia mbinu hii ili kufikisha ujumbe hata kwa wale wasiolewa kiswahili. Katika nyimbo kwa majina *Injili Ni Tamu* na *Imesimama* ametumia lugha yake ya mama ili kuufikisha ujumbe wa injili hadi kwa maajuza walioko vijijini mwao. Ikumbkwe kwamba injili inafaa kusambazwa kwa watu wote na kwa lugha zote.

Katika nyimbo alizoziita Ingia Ndani, God Is Good na Bend This Way ametumia kiingereza ili kuonyesha usomialionao na kutilia mkazo kwenye kufikisha ujumbe wake hata kwa wale wasiokielewa kiswahili. Mtindo huu unabainisha wazi malengo ya msanii husika kutaka kuupitisha ujumbe kwa watu wote bila kubagua lugha wanazozizungumza.

**4.5.3 Kuchanganya Ndimi**

Huu ni ule mtindo wa kuchanganya maneno yaliyo katika lugha mbili au zaidi katika sentensi moja ili kuleta urari wa vina au mizani katika ushairi au hata kuonyesha uhusiano uliopo kati ya lugha inayozungumzwa na jamii husika.

Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma mbinu hii inajitokeza katika nyimbo tatu. Kwenye wimbo aliyoupa jina *Injili Ni Tamu* pale anaimba hivi;

> *"....dance kama mtu amekunywa maziwa.."*

Mstari huu wa maneno unasifia maisha ya uongofu kwamba yeyote aliyempa Yesu maisha yake huwa ni mchangamfu na hujawa na nguvu ambazo mtu aliyekunywa maziwa huwa nazo. Kuyaelezea maisha ya uongofu kwenye maneno haya anaendeleza kusisitiza maudhui ya maisha ya ungofu kwenye wimbo huu.

Maneno ya kwenye wimbo aliyouita *Napenda Mbele* kama;

> "......sema *forward..."*

Matumizi ya mtindo huu kwenye maneno haya yameendeleza maudhui ya maendeleo ya kiuchumi kwenye wimbo huu. Anafafanua nguvu za kiuchumi mtu anazokuwa nazo anapomtegemeaMungu.

Katika wimbo wa *God Is Good* aliposema;

> "....kaa kama *Number Plate* ya gari.."

Mstari huu unaeleza kwa uwazi hali ya maisha ya kiuongofu kwamba hayana siri. Mtu anapookoka matendo yake hudhihirisha hali yake ya maisha ya uungu. Ni katika kutumia mtido huu anaendeleza maudhui ya maisha ya uongofu kwenye wimbo wake.

Christopher Nyangwara Mosioma anapotumia lugha ya kiingereza kwenye mtindo wa kuchanganya ndimi katika nyimbo zake anaonesha usomi kwenye maisha yake ya kawaida. Utumizi wa lugha hii pia unadhihirisha malengo yake ya kufikisha ujumbe kwa vijana ambao mara nyingi ndio hutumia lugha kama hii kwenye mawasiliano yao.

### 4.5.4 Tashbihi

Mtindo huu hurejelea dhana ya ulinganisho wa vitu viwili kwa kutumia maneno ya ulinganisho kwa mfano; kama, ja, mithili ya na kadhalika (Mulokozi 2002). Kulingana na Kahigi (1995), anafafanua tashbihi kama taarifa ya kulinganisha ambayo hutumia maneno haya ya ulinganisho; mithili ya, ja, kama au hata kama kwamba na kadhalika. Kwa upande wake Senkoro(1982), anaileza tashbihi kama utungo wa kitamathali ambao huhusisha ulinganisho wa vitu au watu wawili au hata zaidi kwa kutumia maneno ya ulinganisho yafuatayo; kana kwamba, kama, mfano wa na mengineyo.

Kwa mujibu wa fasili hizi ni wazi kwamba wataalamu hawa wanaitikia kwa kauli zao kwamba tashbihi hufananisha watu au vitu kwa kutumia maneno ya ulinganisho kama; kama, mithili ya,

ja, kana kwamba na kadhalika.Mtunzi wa kazi ya fasihi hutumia mbinu hii kusisitiza sifa za kile anachozungumzia ile kuweka wazi sifa hio au hata kuiongezea chumvi.

Mbinu hii inajitokeza katika nyimbo za injili za Christopher Nyangwara Mosioma kama ifuatavyo:

Katika wimbo aliouita *Injili Ni Tamu* anatumia maneno kama;

"...ruka kama chura...", "*... dance like a snake..." (*cheza kama nyoka)

na

*"...dance like a frog...."* (cheza kama chura),

Anatumia mtindo uo huo pia kwenye wimbo wa *God Is Good* pale alipotumia maneno kama;

".....kaa kama *number plate* (nambari ya usajili) ya gari.."

Christopher Nyangwara Mosioma ameitumia mbinu hii ili kuufikisha ujumbe kwa kuwalenga hasa vijana ambao kwa kiwango kikubwa huitumia mbinu hii ya lugha kwenye mazungumzo yao ya kila siku.kwa kufanya hivyo amefikisha maudhui ya nyimbo zake kwa hadhira mahususi aliyoilenga hasa.

Mount Kenya University

### 4.5.5 Unukuzi kutoka Vitabu Takatifu

Mtindo huu hurejelea dhana ya mtunzi wa kazi za fasihi kunukuu baadhi ya matukio kutoka katika vitabu vitakatifu vya dini. Tukirejelea mhimili wa pili wa kitaja na kitajwa tunapata misimbo miwili ya kimatukio na kiutamaduni. Msimbo wa kimatukio hurejelea matukio ya kiishara ambayo husheheni matendo na visa. Mara nyingi visa vinavyosimuliwa katika kazi za kifasihi za kidini ni visa vinavyonukuliwa kutoka katika vitabu vya kidini. Katika msimbo wa Kiutamaduni, ni kawaida desturi kwa wakristo kusoma na kunukuu kitabu kitakatifu cha Biblia.Nukuzi hizi zinaweza kuhusisha visa, matukio au hata badhi ya maneno kutoka vitabu vya kidini. Unukuzi kutoka vitabu takatifu umedhihirika katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma kwa njia zifuatazo:

Katika wimbo wa *Yesu Nimwagie* amenukuu baadhi ya maneno yake kutoka kitabu cha Biblia cha Mathayo 6:9-13 ambapo anakariri sala ya bwana katika wimbo huo; anaanza kwa kusema '....baba yetu wa mbinguni, mapenzi yako yatimizwe...."

> *"………….. Baba yetu uliyembinguni, jina lako litukuzwe, Ufalme wako na uje,mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu, utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu na utukufu, hata milele. Amina."*
>
> ***Mathayo 6:9-13***

Mtindo huu pia unajidhihirika katika wimbo wa *Imesimama* pale anaposimulia visa vya Ayubu kutoka kitabu kizima cha Ayubu na kisa cha Naomi kutoka kitabu cha Ruthu 1:16 kwenye Biblia.

> *"Naye Ruthuu akasema, Usinisihi nikuache, nirejee nisifuatane nawe; maana wewe uendako nitakwenda, na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu wangu; Pale utakapokufa nitakufa namin na papo hapo nitazikwa; Bwana anitende vivyo na kuzidi, ila kufa tu kutatutenga wewe nami."*
>
> ***Ruthu 1:16.***

Anaendeleza mtindo huu wa unukuzi kutoka kitabu takatifu cha Biblia katika wimbo wa *Yesu Panua* pale anaposimulia kisa cha Kaini na Abel kutoka kitabu cha Mwanzo 4:2-16;

> *".......Habili alikuwa mchunga kondoo, na Kaini alikuwa mkulima ardhi. Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana. Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. Bwana akamtakakabali Habili na sadaka yeke bali Kaini hakumtakakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhabika sana, uso wake ukakunjamana. Bwana akamwambia Kaini, kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana? Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde. Kaini akamwambia Habili nduguye,[ Twende uwandani] Ikawa walipokuwapo uwandani, Kaini akamwinukia Habili nduguye, akamwua...."*
>
> ***Mwanzo 4:2-16***

Ni katika wimbo uo huo pia anaposimulia hadithi ya Nuhu cha kujenga safina kutoka kitabu cha Biblia cha Mwanzo 6:13-19;

> *"Mungu akamwambia Nuhu, Mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia. Ujifanyie safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami. Hivi ndivyo utakavyoifanya; mikono mia tatu urefu wa safina, mikono hamsini upana wake, na mikono thelathini kwenda juu kwake. Uifanye safina mwangaza, ukaumalize juu kiasi cha mkono mmoja; ukautie mlango wa safina katika ubavu wake; ukaifanyie dari tatu, ya chini, ya pili ya tatu. Na tazama, nitaleta gharika ya maji juu ya nchi, niharibu kila kitu chenye mwili wa pumzi ya uhai, kisiwepo chini ya mbingu; kila kilichoko duniani kitakufa. Lakini nitafanya agano langu nawe kuwa thabiti, nawe utaingia katika safina, wewe na wanao, na mkeo, na wake za wanao, pamoja nawe. Na katika kila kilicho hai chenye mwili, wawili wa kila namna utawaleta ndani ya safina, kuwahifadhi pamoja nawe; wawe mume na mke."*
>
> ***Mwanzo 6:13-19***

Ni katika kutaka maisha yake kupanuliwa katika wimbo aliyouita *Yesu Panua* aliposhirikisha kisa cha Daudi na Goliathi kutoka kitabu cha 1 Samuel 17:45 - 47.

> *"Ndipo Daudi akamwambia yule Mfilisti, wew unanijilia mimi na upanga, na fumo, na mkuki, bali mimi ninakujia wewe kwa jina la Bwana wa majeshi, Mungu wa majeshi ya Israeli uliowatukana. Siku hii ya leo Bwana atakuua mkononi mwangu, nami nitakupiga, na kukuondolea kichwa chako, nami leo nitawapa ndege wa angani na wanyama wa nchi*

*mizoga ya majeshi ya Wafilisti, ili kwamba dunia nzima wajue ya kuwa yuko Mungu katika Israeli. Nao jamii ya watu wowte pia wajue ya kwamba Bwana haokoi kwa upanga wala kwa mkuki; maana vita ni vya Bwana, naye atawatia ninyi mikononi mwetu."*

***1 Samuel 17:45 – 47.***

Mbinu hii pia anaiendeleza katika wimbo wa *Bend This Way* anaposimulia kisa cha Abraham na Sara kutoka kitabu cha Mwanzo 12 na kisa cha Daudi mchunga kondoo kutoka kitabu cha Samuel 17:15 - 47.

*" Bwana akamwambia Abramu, toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha. Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa na kukubariki na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka....."*

***Mwanzo 12:1 – 2***

Katika kunukuu kitabu kitakatifu cha Biblia, msanii Christopher Nyangwara Mosioma alinuia kuweka bayana misingi ya imani yake ya kikristo. Ikumbukwe kwamba katika mafundisho ya dini ya kikristo misingi yake hutokana na maandiko yaliyokwenye Biblia takatifu. Visa kutoka kwa Biblia alivyovishirikisha kwenye nyimbo zake alikusudia viwatie imani wasikilizaji wa nyimbo zake kwamba nao siku yao ya mafanikio itafika.

### 4.5.6 Sitiari

Mbinu hii huhusisha ulinganisho wa vitu viwili moja kwa moja bila kutumia maneno ya ulinganisho. Tukirejelea tena mhimili wa pili wa kitaja na kitajwa tunaegemea msimbo wa Kiurejelezi. Msimbo huu hurejelea dhana ya kufananisha moja kwa moja. Ufananisho huu huhusisha sifa za kibinadamu ambazo hupewa wahuska katika kazi ya fasihi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira. Mtindo huu hulenga kutilia mkazo na kusisitiza mwingiliano wa muonekano na kufanana kwa kiwango kikubwa kati ya vitu vinavyofananishwa.

Mount Kenya University

Kulingana na Mulokozi 2002, anafasili sitiari kama tamathali ya semi ambayo hutumiwa kutengeneza taswira fulani inayodhihirisha athari au hata kuzindua mwitikio fulani kwa mtazamo wa hadhira. Kulingana na kauli hii ni sawa kusema kwamba sitiari hulinganisha vitu au watu kwa misingi kwamba vipo sawa kimuonekano au kisifa. Huhusisha namna ya kuhamisha maana kutoka dhana au kitu mpaka kwa dhana au kitu kingine. Dhana ya kimaana inayohusishwa hapa mara nyingi huwa na utofauti hasa kwa kuegemea sifa zinazohusisha semantiki moja ya msingi. Kama Kahigi 1995, alivyosema, kinacholinganishwa hapa ni muonekano au mienendo au matumizi ya kitu kwa kuangazia uhusiano uliopo katika muonekano au matumizi ya kitu kingine. Kwa mfano; Juma ni simba kumaanisha kwamba mambo anayoyafanya Juma yanaonyesha ujasiri kama ule wa simba nyikani.

Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma mtindo huu unadhihirika katika wimbo wa *Yesu Nimwagie* pale anapomrejelea Yesu kama 'Simba wa Yuda" akitaka kuonyesha ujasiri wake wa kufanya na kushiriki katika mambo ya kutisha ya duniani kwa hali ya kutoshindwa.

Anaendeleza mbinu hii pia katika wimbo wa *Napenda Mbele* pale msanii mwenyewe anaposema kwamba yeye ni "Simba wa kike" na kwamba akinguruma hutisha. Maneno haya yanadhihirisha kujifananisha na ukali wa simba unaotia uoga maadui wake. Ukali huu anajivunia kupewa na Mungu katika misingi yake ya imani.

### 4.5.7 Jazanda

Mtindo huu hurejelea matumizi ya lugha fiche ya kimafumbo katika kuelezea mambo ambapo maneno huteuliwa kwa ustadi mkubwa katika hali ya kumfikirisha msikilizaji, mtazamazi au hata msomaji wa kazi ya fasihi. Katika mhimili wa kitaja na kitajwa tunapata misimbo ya kiseme na kimatukio. Msimbo wa kiseme unaangazia maana ya matumizi ya maneno kisemantiki ilihali

msimbo wa Kimatukio hurejelea dhana ya matukio ya kiishara. Misimbo hii miwili mara nyingi huendana moja kwamoja na matumizi ya kijazanda katika fasihi. Huenda mambo yanayoangaziwa katika jazanda husika yawe tofauti kabisa na mambo yanayojitokeza katika maana ya juu ya jazanda yenyewe.

Mbinu hii imetumika kwa kiwango kikubwa katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma kama ifuatavyo:

Katika wimbo wa *Nataka Nikuingize* msanii huyu anatumia jazanda akisema, *"......hata nikiinama.....nikiinuka mbele......nikiinuka nyuma......napata raha akiwa ndani.."* Hapa anamaanisha hata akiwa katika panda shuka za maisha ya mwanadamu ya kila siku havunjiki moyo kwa kuwa Mungu yupo ndani yamaisha yake. Jazanda pia anaiendeleza pale anaposema, *" kwa Yesu kuna asali..."* akimaanisha kwamba maisha ya uongofu ndani ya Yesu yamejawa mazuri na matamu yasiyo na matatizo.

Katika wimbo wa *Napenda Mbele* anasema, *".....nyuma kuna vumbi na giza...."* maneno haya ni ya kijazanda kwani anarejelea shida na taabu zinazopatikana katika maisha pale mtu anapokuwa na udhaifu usiyomruhusu kwenda mbele kimaisha bali kumbakisha nyuma kwenye shida zake anazozifanisha na vumbi na giza.

Katika wimbo wa *Ingia Ndani* anasema, *".....ukiingia ndani kuna baraka na uzima wa milele...."* maneno haya yanaashiria mtu kuwa katika maisha ya uongofu ili kupata baraka kutoka Mungu na kujiepusha na madhila ya dunia hii daima. Anaendeleza jazanda akiuliza, *"......hupendi matope na uliumbwa na matope...?"* akirejelea shida za dunia kama matope na kwamba miili yetu imeumbiwa shida na kwa hivyo hatupaswi kuziogopa kwani ni mojawapo ya

nguzo zinajenga maisha yetu hapa duniani na kwamba ni matatizo ya muda tu kwani tope likioshwa hutokomea.

Kwenye wimbo wa *Yesu Panua* anatumia neno “panua” kuleta dhana ya muumini anayemtegemea Mungu kufunguliwa njia za kufauli maisjhani na kumiminiwa baraka na hata kusema *“....nasikia nikugonge.....,ukicheza na neno utagongwa.....”* kumaanisha kwamba mipango ya Mungu hakuna wa kuipinga kwani hakuna binadamu mwenye uwezo huo.

Jazanda pia inajitokeza katika wimbo wa *Bend This Way* anaposema *“...bisha utafunguliwa.....*” kwamba mambo yako yanapoenda kisegemnege uanpomwita Mungu hakika anakulainishia mambo yako. Anwani wa wimbo wenyewe “*Bend This Way*” ni jazanda kwani inaashiria kule kuinama kwa nia ya kutoa heshima na kunyenyekea kwa mtu ili kupata msaada.

Mtindo huu wa kimafumbo pia unajitokeza katika wimbo wa *Tuko Uchi* pale anwani yenyewe pia inarejelea hali ya kutokuwa na siri mbele za mwenyezi Mungu kwani anafahamu mambo yote mabaya na mazuri tunayoyafanya.

### 4.5.8 Usimulizi

Hii ni mbinu ya utunzi wa kisanaa ambapo mtunzi huelezea matukio katika kazi yake ya usanii kwa njia ya masimulizi kama mtu asimuliaye hadithi. Usimulizi hushikisha matukio, matendo na visa kwenye kufikisha ujumbe. Ushirikishi huu wa mambo haya matatu yanaegemea kwenye uchambuzi wa mhimili wa kitaja na kitajwa kwenye msimbo wa Kimatukio. Masimulizi husimulia visa vilivyosheheni matukio yaliyobeba mafunzo ya kifasihi ili kuufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Mbinu hii hukuza umakinifu kwa hadhira yake na kuiburudisha na hata kuufikisha ujumbe uliokusudiwa.

Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma anatumia mbinu hii ya usimulizi katika nyimbo kama *Yesu Panua* pale anavyoendeleza hadithi za Kaini na Habili.

> *Hadithi hii inawahusisha wana wawili wa Adam na Hawa ambao ni Kaini na Habili. Kaini alikuwa mkulima aliyekuwa anakuza matunda, nafaka na mboga ilihali Habili alikuwa mfugaji wa kondoo.*
>
> *Siku moja Habili na Kaini waliamua kumletea Bwana Mungu sadaka. Kaini alichukua kiasi cha mazao yake ya shambani na kutolea Mungu sadaka. Habili naye akachagua kondo mmoja mkubwa miongoni mwa kundi alilolifuga ili kumtolea mwenyezi Mungu sadaka. Bwana Mungu akapendezwa na sadaka ya Habili na kuchukuzwa na adaka ya Kaini kwa kuwa Kaini alikuwa na chuki dhidi ya nduguye.*
>
> *Kaini alipogundua hivyo, alimdanganya nduuguye Habili na kwenda mahali pasipokuwa na mtu yeyote mwingine na kumpiga nduguye hadi akamtoa uhai. Na kwa hayo Habili akawa binadamu wa kwanza kuonja mauti.*

Christopher Nyangwara Mosioma ametumia masimulizi ya hadithi hii kuihimiza hadhira yake dhidi ya madhara ya chuki na wivu miongoni mwa wanajamii. Katika mchakato mzima wa kuidondoa hadithi hii husika kutoka kwenye Biblia alinuia kuleta uzito wa chukizo kutoka kwa Mungu dhidi ya chuki baina yetu. Tukijikita pia kwenye mafunzo ya hadithi hii anajaribu kuleta shime kwenye kutoa sadaka kwa Mungu. Anajenga misingi ya utoaji kwenye hadhira yake ili kudhihirisha shukrani kwa Mwenyezi Munngu na kwamba kila tunapotoa sadaka tuitoe kwa moyo mmoja.

Embarambamba anaendeleza mtindo huu wa masimulizi pale anaposimulia kisa cha Nuhu kujenga safina katika wimbo aliouita *Bend This Way*.

> *Kisa hiki kinamhusisha Nuhu akiwa na mke na wana watatu. Majina ya watoto wa Nuhu yalikuwa Shemu, Yafeti na Hamu. Watoto hawa wa Nuhu walikuwa wameoa na kuishi na familia zao.*
>
> *Katika maisha yake ya kumtukuza Mungu, akaagizwa na bwana Mungu kufanya jambo lisilokuwa la kawaida. Aliagizwa kuijenga safina iliyokuwa na ukubwa wa kustaajabisha kwani ukubwa wake ulifananishwa na meli na kwa mbali ilionekana kama sanduku lililokuwa na urefu mkubwa mno.*

*Mwenyezi Mungu alimuamuru kujenga safina yenye urefu wa vyumba vitatu kwenda juu na kuigawanya vijumba ndani yake ili yeye Nuhu na jama yake, chakula na wanyama wapate nafasi zao. Nuhu aliagizwa kuikaza safina hio kwa ustadi mkubwa ili ikapambane na nguvu za maji kwani alikuwa amemtahadharisha kwamba ataleta gharika kubwa ili kuuangamiza ulimwengu mzima. Bwana Mungu alimhakikishia Nuhu kwamba kila atakayekuwa nje ya safina hio atakayoijenga ataangamia.*

*Nuhu na jamaa yake walishirikiana kuijenga safina usiku na mchana kama alivyoagiza Mwenyezi Mungu huku wakinyimwa na msaada wowote na watu wengine wakiwabeza na kuwakejeli wakizidi kutenda maovu. Ujenzi ule wa safina uliwachukua muda mrefu kuimaliza. Na hata baada ya miaka mingi safina ilimalizika na Mungu akamuamuru Nuhu waingize wanyama ndani ya safina pamoja aina zote za ndege akizingatia kuwepo kwa jinsia zote mbili. Mwishowe Nuhu na familia yake wakaingia ndani ya safina na Mwenyezi Mungu kwa nguvu zake mwenyewe akafunga lango la safina ile.*

*Kwa imani waliokuwa nayo Nuhu na familia yake, waliingia ndani na kusubiri ahadi ya Mwenyezi Mungu. Watu waliouwa nje ya safina walizidi kufanya matendo yao maovu na kukejeli kitendo cha Nuhu na familia yake kufingiwa kwenye safina. Haikuchukua muda mrefu kicheko chao kilifika ukingoni.*

*Baada ya kipindi cha muda mfupi maji yalianza kumiminika kutoka mawinguni kama vile yamwagikavyo kutoka kwa ndoo. Wale watu waliokuwa nje ya safina wakaanza kusemezana na kusadiki maneno aliyoyasema Nuhu alipokuwa akijenga safina. Maji yakaanza kuunda vibonde, vibonde vikawa kama mitona mito hio ikaungana na kuwa kama bahari.*

*Nguvu za maji yaale zikaangusha miti, zikapindua mawe na kuyeyusha udongo milimani kwa nguvu yake. Maji yalizidi kumwagika kutoka angani kwa siku arubaini usiku na mchana. Watu waliokuwa nje ya safina wakaanza kumlilia Nuhu awafungulie safina ili waweze kuingia ndani ila haikuwezana kwani Mungu ndiye aliyekuwa ameufunga na Nuhu hakuwa na uwezo huo.*

*Baada ya kipindi hiki Mwenyezi Mungu alileta upepo ambao uliyakausha maji kwa haraka na baada ya miezi mtano hivi safina iliweza kutulia juu ya mlima mmoja mkubwa na kila siku ziliposonga nayo maji yaliendelea kupungua. Waliokuwa nje ya safina wote waliangamia kwa maji.*

*Nuhu alipokea ishara ya kukauka kwa maji kupitia njiwa aliyemtoa na kurudi akiwana jani la mzaituni kinwani kuashiri akuwa nchi ilikuwa shwari. Alifanya hivyo mara tatu na kwa mara ya tatu njiwa yule hakurudi tena kwenye safina ishara tosha ya maji kukauka kabisa.*

*Mwenyezi Mungu akamuamuru Nuhu na familia yake pamoja na wanyama waliokuwa ndani ya safina kutoka nje baada ya kipindi cha mwaka mmoja kutoka mvua ile ya ajabu kuanza.*

Matumizi ya hadithi hii kwenye wimbo husika wa Christpher Nyangwara Mosioma yalitumika kutilia mkazo ubora wa matendo mema na ubaya wa matendo mabaya mbele ya Mwenyezi

Mungu. Embaramba alitaka hadhira yake kufahamu madhara ya matendo maovu kuwa ni mauti. Mwenyezi Mungu hapendi watu wasiotii mafundisho yake. Vile vile hadithii hii aliitumia kutilia mkazo maudhui ya maisha ya kilokole. Maisha ya haya ya kiungu humfurahisha Mungu na kukulinda kutokana hasira zake na kukuweka hai ili uendelee kulitukuza jina lake.

Hadithi ya Daudi na Goliathi pia inatajwa na kusimuliwa katika wimbo uu huu wa *Bend This Way*.

> *Hadithi hii inamhusisha kiongozi mmoja wa wafilisti aliyeitwa Goliathi na kijana mdogo mchunga kondoo wa waisraeli kwa jina Daudi. Daudi alikuwa akichunga kondoo za babake kila siku. Siku hio ya vita Yese alimtuma Daudi kuwapelekea ndugu zake waliokuwa kwa jeshi la Sauli nafaka na mikate na akawajue kwamba ni wazima.*
>
> *Katika shuhuli hio akampata Goliathi akijigamba mbele ya waisraeli akiwauliza kuwa ni nani kati yao amabye yupo tayari kupigana naye. Daudi akamuuliza askari mmoja kuwa mtu atakayepigana na Goliathi angepewa nini na akaambiwa kwambwa mtu huyo anangepewa mali nyingi na Sauli na hata kuozwa binti yake.*
>
> *Naye Daudi alijuzwa kwamba waisraeli wote walimuogopa Goliathi kwani alaikuwa jitu lenye mirama minne mwenye kimo kilichopata mita tatu na aliyekuwa na askari wa kumchukulia ngao yake iwapo ingeanguka wakatii wa vita. Daudi kwa kuyaskia yale,aliomba kupigana na jitu lile na ujumbe ukapelekwa kwa mfalme Sauli.*
>
> *Sauli akamuonya Daudi kwamba Goliathi alikuwa na uzoefu mkubwa wa vita na kwamba yeye Daudi alikuwa mdogo mno asiyekuwa na ujuzi wowote wa kivita. Hata hivyo Daudi hakuvunjika moyo na akajipiga moyo konde kupambana naye.*
>
> *Daudi akateremka kwenye njia iliyoshuka kwenye mto na kuokota mawe matamu amabayo yalikuwa laini na kuyaweka kwenye kifuko alichokuwa amaejifunga kiunoni na kujihami kwa kombeo tayari kwa vita.*
>
> *Goliathi alipomuona Daudi kamjia na mawe na kombeo alimdharau sana lakini Daudi akamwambia kuwa hata kama yeye Goliathi alimjia kwa upanga na mkuki yeye alijiamini kuingia vita vile na jina la Yeheova. Akachukua jiwe moja kwenye kifuko chake na kumrushia Goliathi kutumia kombo na kumpiga kicwani, naye Goliathi akaanguka chini na kufa papo hapo. Nao wafilisti walipoona hayo walitoroka na kuwaachia waisraeli ushindi wa vita hivyo.*

Matumizi ya hadithi hii kwenye wimbo huu yalikusudua kujenga misingi kkatika maudhui ya ukuu wa Mungu kwenye maisha yetu. Embaramba alinuia kuweka wazi uwezo aliyonao Mwenyezi Mungu kwenye maisha hata ikiwa yaliyoko mbele yetu tunayaona hatuyawezi.

Ilimchukua Daudi kuwa na ujasiri ili kushinda vita vile kwa kuamini uwezo wa Mungu kwenye vita vile na akaibuka mshindi.

Katika kuonyesha na kukuza maudhui ya imani ya kidini, Embaramba anatumia kisa hiki kuonyesha kwamba tunapomtegemea Mungu kamwe hatuwezi kuaibika na tutashinda majaribu yetu. Watu waliokuwa karibu na Daudi walimutia uoga na hata kumtahadhari kujihusisha kwenye vita vile lakini yeye alimtumainia Mungu na kuamini kwamba atashinda.

Hadithi hii inawahimiza wakristo kuendelea kumtumania Mungu katikka kila wafanyalo kwani watafaulu kwa lolote wanapoweka imani kwa Mungu.

Embaramaba anaendeleza Mtindo huu wa usimuizi pale alipotaja na kusimulia matukio katika hadithi ya Abraham na Sara kwenye wimbo uo huo wa *Bend This Way*.

> *Matukio ya hadithi ya Abraham na Sara inawahusisha wawili hao kuwa walioana kwa miaka mingi na kukaa bila kupata mtoto. Walikuwa wameiacha nchi yao iliyojulikana kama Uru na kuhamia kwenye mahema. Sara alikuwa amekaa muda mrefu akitamani mtoto na mwishowe akamwambia mumewe Abraham kuweza kulala na kijakazi wake aliyekuwa akiitwa Hagari ili kupata mtoto naye. Alimuahidi mumewe kwamba angemchukulia mtoto huyo kama wake.*
>
> *Baada ya kipindi kisichokuwa kirefu, Hagari alipata mtoto na kumuita Ishameli. Baada ya miaka mingi Abraham alipokuwa na miaka tisini na tisa na Sara akiwa na miaka themanini na tisa, mwenyezi Mungu aliwatunuku mtoto wa kiume nao wakamuita Isaka.*
>
> *Siku moja mwenyezi Mungu aliamua kumjaribu Abraham. Alimuamuru amchinje na kumteketeza mwanae Isaka kama sadaka. Walipoenda mlimani kufanaya hivyo, Mwenyezi Mungu alimpa Abraham kondoo wa kuchinja kwa njia ya miujiza na kumnusuru Isaka.ikumbukwe kwamba Abrahamu alikuwa tayari kufanya vile alivyoagizwa na Mwenyezi Mungu na Mungu akapeipenda imani ya Abraham.*

Matumizi ya usimulizi wa hadithi katika wimbo husika, yamelandana na maudhui ya wimbo huo. Katika jazanda inayopatikana kwenye kichwa cha wimbo “Bend This Way” kuashirikia kumtii Mwenyezi Mungu. Ni kutokana na kumtii Mwenyezi Mungu ndipo Abraham akaweza kupata mtoto akiwa na umri mkongwe sana.

Hadithi hii imekuza maudhui ya ukuu wa Mungu pale ambapo ukuu huu umewawezesha Abraham na mkewe kupata mtoto ijapokuwa walikuwa wazee kupindukia. Uwezo huu wa kipekee unadhihirisha matendo makuu ya Mungu kwa watu wanaomtii na kufuata maagizo yake. Maudhui mengine aliyoyakuza kutumia masimulizi ya hadithi hii ni imani ya kidini. Ni kutokana na imani aliyokuwa nayo Abraham ambapo bwana Mungu alipendezwa naye na hata kumtunuku mwana kondoo wa kumtoa sadaka badala ya Isaka.

Christopher Nyangwara Mosioma alinuia kuwapa walokole tumaini la kuendelea kuzidi kumtumania Mungu katika maisha yao ya kila siku kwani Mungu anapendezwa na hilo. Katika mafundisho ya kikristo, wanaamini kwamba Abraham ni baba wa imani kutokana na hadithi hii na wanamfatilia sana katika imani yao juu ya Mwenyezi Mungu.

Utumizi wa masimulizi katika fasihi huboresha umakini wa hadhira kwa kile kinachowasilishwa kwao na kujenga uhusiano bora baina ya mwasilishaji na hadhira yake. Dhima ndio iliyompelekea Christopher Nyangwara Mosioma kuitumia mbinu hii katika nyimbo zake ili kuboresha uwasilishaji wa kaze zake kwa hadhira lengwa. Ni dhahiri kwamba hadithi alizozitumia msanii huyu kwenye nyimbo zake zimeweka wazi maudhui aliyokusudia kuyawakilisha kwa hadhira yake. Ikimbukwe kwamba katika matumizi ya wasika kwenye masimulizi ndipo maudhui yaliyolemgwa kuwasilishwa kujengwa na kujidhihirisha kwa uwazi. Mambo haya huonekana kuendana na kushabihiana moja kwa moja na kwamwe haya tangamani. Ni kutokana na hayo ndipo ujumbe hupitishwa vyema.

### 4.5.9 Uteuzi wa maneno

Mbinu hii hurejelea uteuzi wa maneno katika kuuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Msanii huteua maneno katika kuzua ishara mbalimbali kwenye kazi yake. Uteuzi huu huzua maana mbalimbali kulingana na tamaduni za jamii husika. Neno moja katika mazingira fulani ya kifasihi linaweza

kuzua ishara au tafsiri tofauti tofauti kulingana na maana au ishara inayohusishwa na mazoea ya utumizi wake na hadhira husika. Hali ya tafsiri ya neno inaelezwa wazi na mihimili ya nadharia ya simiotiki. Mhimili wa kwanza unaeleza kuweko kwa matumizi ya ishara katika kila neno ili kuleta maana ya kizumzwacho.

Mhimili wa pili unabainisha uhusiano uliopo wa kinasibu na kueleza kwamba maana hubadilidika kutoka lugha moja hadi nyingine hata ikiwa neno linabaki lile lile. Mhimili huu wa pili una misimbo inayorejelea kwa karibu sana msimamo huu. Mhimili wa Kihemetiki unaegemea maelezo yanafungamana kupata maana kutokana na anwani ya kazi husika ya fasihi. Hadhira hupata picha kamili kutokana tu na kusoma anwani ya kazi husika na kwa muhtasari tu inaweza kujua kinachozungumziwa kwenye kazi hio.

Vile vile katika msimbo wa Kiseme, maneno yaliyotumiwa katika kazi fulani ya fasihi yanaweza kuwa yametumiwa kwa njia ya kimafumbo ili kumanisha mambo tofauti kabisa. Kwa kuegemea msimbo huu maneno katika kazi ya fasihi yanaweza kutumiwa kisemantiki ili kufikisha ujumbe kwa ya kimafumbimafumbo.

Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma ametumia maneno mengi yanayo leta maana tofauti tofauti katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Baadhi ya maneno haya ni kama; *bend this way* (inama hivi), tuko uchi, Yesu ninyonye, napenda mbele, ingia ndani, Yesu panua, injili ni tamu, Yesu nimwagie, imesimama, na nataka nikuingize.

Katika uteuzi wa maneno ili kuumba anwani za nyimbo zake, Christopher Nyangwara Mosioma aliteua kimakusudi maneno yaliyozowelewa na vijana kwenye mikatadha yao ya kidunia, ili kuwavutia kusikiza nyimbo zake.

Nikianza kuangazia anwani ya wimbo aliouita *Bend This Way*, katika tafsiri sisisi ukimaanisha "inama hivi," anwani hii imetumiwa kuibua maelezo ya kijazanda yanayohusisha kutii kanuni za Mwenyezi Mungu maishani. Anaendeleza kusisitiza kauli hii pale anaporudiarudia maneno haya ili kuufikisha ujumbe aliokusudia. Ikumbukwe kwamba ishara moja yapo ya kuonyesha kutii na heshima ni kumuinamia mtu. Jambo hili huleta athari ya moja kwa moja ya mdhaifu mbele ya yule unayemuinamia nalo ndilo lengo hasa la Embarambamba kuyatumia maneno haya kwenye anwani ya wimbo huu, ili kumuonyesha binadamu iwapo anataka kufaulu maishani hana budi kumtii Mungu.

Katika matumizi ya kikawaida ya vijana, "Bend This Way" inachukuliwa kumaanisha maana tofauti kabisa. Kulingana na tafsiri ya vijana maneno haya yanachukuliwa kumuamrisha mpenzi wako hasa wa kike wakati wa tendo la ndoa "kuinama kwa namna itakayokuridhisha kwa kusudi la tendo hilo." Ikumbukwe kwamba msanii Christopher Nyangwara Mosioma anawafahamu na kutangamana na vijana wanaoegemea maana hii, kwa hivyo matumizi ya maneno haya husika kwenye wimbo huu na hata matumizi yake kwenye kuiunda anwani yake aliwalenga hasa vijana kuvutiwa na kusikiliza wimbo huu. Matumizi ya maneno haya yamekusudiwa kuitia hamu hadhira lengwa kutaka kusikiliza wimbo huu na kupigwa na butwaa pale wanapopata kinachoimbwa ni tofauti na ukawaida wa wanachodhania.

Pili, katika mchakato wa kuyateua maneno ya anwani wa wimbo "*Tuko Uchi*," alikuwa na msukumo uu huu mmoja. Katika tafsiri ya kikawaida, neno " uchi" linamaanisha kutokuwa na nguo na kuwa kama ulivyozaliwa. Maana nyingine kulingana na matumizi ya kinahau kama vile "kuvuliwa nguo hadharani" kumaanisha kuaibishwa au kuweka aibu ya hadharani kwa nia ya kumdhalilisha. Christopher Nyangwara Mosioma alitumia maneno haya kijazanda kuelezea vile tunavyoonekana mbele za Mungu kulingana na tunayoyafanya kinyume na mafundisho ya

Mungu. Ainuia kueleza ukuu wa Mungu ambao una uwezo wa kuyafahamu maovu yote ambayo tunayafanya kwa kificho tukidhani hakuna anayetuona.

Tunapoegemea kwenye sifa, mazoea na desturi za uteuzi wa maneno katika sajili ya kidini. Anwani hii inakengeuka kabisa sifa hizo. Ikumbukwe kwamba kati ya sifa za msamiati wa kidini ni kusheheni kwa maneno ya adabu na unyenyekevu. Anwani hii katika mazingira ya utafsiri wa kawaida inaleta aibu na kuvunja miiko hasa shughuli za kiibada ambazo hushirikisha watu wa umri tofauti tofauti bila kubagua watoto. Dhana ya watu kuwa uchi inaleta kuhamishwa kwa fikra za kiungu na kuleta hali ya kidunia iwapo kutatoweka umakini na uelewa wa kinachozungumziwa.

Tukiendelea kuangazia uteuzi wa tatu wa maneno, tutaangazia maneno yaliyoteuliwa kuumba anwani ya wimbo aliyouita "*Yesu Ninyonye*." Maneno haya pia kwa namna ya kijazanda kama alivyoyanuia kuyatumia. Christopher Nyangwara Mosioma alikusudia kuzua dhana ya kusamehewa dhambi ( "kunyonywa" ), akimanisha haitojalisha ni matendo mangapi ya dhambi uliyafanya kwani Mungu ana uwezo wa kufuta dhambi mara moja."Unyonyaji" wa dhambi hizi unakusudiwa kuonyesha uharaka na uwezo wa kipekee wa kufanywa kwa jambo kwa sababu ya ukuu na uwezo alionao Mwenyezi Mungu.

Kulingana na tafsiri ya Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja toleo la nne, neno "nyonya" litafsiriwa kama kitendo cha kuvuta kitu cha majimaji kwa kutumia mdomo, kama ndama au mtoto afanyavyo maziwa ya mama yake. Maana hii iliyotafsiriwa hapo juu ndio inayozua utata katika tafsiri ya wanajamii kwenye matumizi yao ya neno hilo hata kuleta mjadala kwenye Kamati ya hati miliki ya wanamziki nchini Kenya.

Kulingana na matumizi na muktadha wa wanavyotumia neno hili, dhana inayodhihirishwa na kupachikwa nao ni ile ya kuashiria kufyonza utupu wa mpenzi wako ili kumuandaa kwa tendo la ndoa. Msanii Christopher Nyangwara Mosioma anakariri neno " kunyonywa" kwenye korasi ya wimbo huu ili kuinasa hadhira yake kwenye kusudio tofauti na kile walichozoea kupachika kwenye tafsiri ya neno hili.

Urudiaji huu wa neno hili husika unawafanya wasikilizaji wa nyimbo zake kupata burudani ya fikra hasa pale wanapojua walichozoea kudhania kwenye maana ya neno hili si kile kinachoimbwa na msanii husika jambo linalowapelekea kufanya mzaha wanapouimba wimbo wenyewe. Athari hii inasababisha kufanikishwa kwa lengo la msanii husika kupata kuwaathiri vijana ili wawe na hamu ya kusikiliza nyimbo zake kwa kiwango cha juu.

Katika kuteua maneno ya anwani za nyimbo zake, Christopher Nyangwara Mosioma anatumia baadhi ya msamiati wa lugha za vijana na kuumba anwani ya wimbo " Napenda Mbele." Kulingana na vile alivyoeleza matumizi ya maneno haya kwenye wimbo wake, alinuia kueleta dhana ya kuinuka kiuchumi na kuwa mtu tajika mbele ya watu. Anasisitiza dhana hii ya kuinuliwa kiuchumi pale anaposema "kupenda mbele" kwake ni kwa sababu ya kuwa " nyuma" kuna vumbi na madharau. Kauli hii inadhihirisha hali ya kuwa na dharau na mateso pale mtu anapokuwa hana uwezo wa kiuchumi na hata mchafu wa mwili.

Lengo la msanii husika kutumia msamiati wa lugha ya vijana ili kuwavutia kusikiliza nyimbo zake ni jambo linaloleta utata kwenye kuielewa nyimbo hii hasa kwenye ujumbe unaopitishwa na anwani ya nyimbo. Kulingana na tafsiri na wanavyoifasili anwani ya nyimbo husika ni kwamba "kupenda mbele" kunahusishwa na mtu kupenda tendo la ngono. Hali inayoleta

sintofahamu hata kwenye kiwango cha lugha ya adabu na heshima kilicho kwenye nyimbo za Christopher Nyakwara Mosioma (Embarambamba).

Christopher Nyangwara Mosioma anatumia msamiati huu wa vijana kuupa anwani wimbo wake mwingine kwa jina " Yesu Panua." Kulingana na alivyokusudia kwenye muktadha wa mazingira ya matumizi ya maneno haya kwenye wimbo wake, msanii huyu husika ananuiia kuleta dhana ya kujiendeleza kimapato na kuwa na upana mrefu wa kiwango cha kifedha.

Sintofahamu inatokea tu pale ambapo anarudiarudia neno " panua" mara nyingi likiwa kivyake na kuleta fikra tofauti kwa hadhira yake lengwa ambayo ni vijana. Katika tafsiri ya kamusi ya karne ya ishirini na moja toleo la nne, neno Panua lina maana ya kufanya kuwa kubwa kwa upana au kuongeza kwa nia ya kutanua.

Tafsiri hii inaendana moja kwa moja na tafsiri ya lugha ya vijana ambao mara nyingi lugha zao husheheni msamiati mwingi wa kurejela mambo machafu. Msamiati huu wa kurejelea vitu vichafu kimaadili hutumia maneno ya kawaida ili kuficha ukali wa kile wanachorejelea. Kwa maalezo haya, neno panua kama lilivyoelezwa na kamusi ya karne ya ishirini na moja, vijana wanalitumia neno hili kurejelea dhana ya kuweka mguu wa kulia na kushoto na mwingine kwa nia ya kuruhusu kupenyezwa kwa utupu wa kiume kwenye utupu wa kike. Kwa sababu ya tafsiri hii ya vijana, urudiajirudiaji wa neno hili peke yake kwenye wimbo husika unawatia vijana mawazo hasi ya kingono kuliko mawazo ya kitakatifu au ya kiungu.

Ni katika mchakato uu huu mmoja wa kutumia msamiati wa lugha ya vijana, ambapo Embarambamba anatumia neno "Nimwagie" kwenye kuumba anwani ya wimbo wake mwingine. Neno "nimwagie" limetokana na kuambishwa kwa neno "mwaga" ambalo kulingana na tafsiri ya kamusi ya karne ya ishirini na moja toleo la nne lina maanisha kutoa kitu cha

majimaji, punjepunje au unga ndani ya kitu kingine na kukitawanya. Kulingana na alivyolitumia neno hili, Embaramba alilitumia ili kusisitiza dhana ya kutaka kumiminiwa baraka na Mwenyezi Mungu. Wingi huu wa baraka hizi ndio uliompelekea yeye kuuwekea dhana ya kumiminiwa ili kusisitiza ukuu wa Mungu.

Katika msamiati wa lugha ya vijana neno “nimwagie” linadhihirisha dhana tofauti kabisa. Neno hili husika limelimbikiziwa tafsiri ya kingono inayorejelea kufika kileleni kwa mwanaume wakati wa tendo la ndoa. Tafsiri hii inawepekelea vijana kuwa na mawazo tofauti kabisa kwenye kuuimba wimbo huu kinyume na dhima ya kuimbwa kwa nyimbo za kidini.

Msanii christopher Nyangwara Mosioma alitumia mbinu hii pia kwenye uteuzi wa msamiati na kuuita wimbo wake  mmoja “imesimama.” Kulingana na kinachoimbwa na kusisitizwa kwenye wimbo hu, ni nguvu za mipango ya Mungu kutobadilishwa na mtu yeyote mwingine. Sifa hii ina kuza maudhui ya ukuu wa Mungu nakwamba hakuna yeyote awezae kulipinga neno lake.

Kamusi ya karne ya ishirini na moja toleo la nne inatafsiri neno “simama” kumaanisha kuwa wima kwa kutegemea miguu au kitako cha kitu yaani kuinuka. Neno hili katika tafsiri ya lugha ya vijana na kutegemea miktadha yao ya matumizi, wanalitumia kuleta dhana ya kuwa tayari kwa uume wa mtu ili kufanya tendo la ndoa; kusimika.

Embarambamba analitumia neno hili na kulikariri likiwa kivyake kwenye korasi ya wimbo huu na kuwapagawisha vijana wanaosikiliza nyimbo huku akiwaweka fikra tofauti na ile aliyonuia kuiwasilisha kwao ya kuneza injili.

Christopher Nyangwara Mosioma  anaendelea kuteua msamiati tatanishi pale anapouita wimbo wake mmoja “Nataka Nikuingize.” Wimbo huu anautelia maneno yanayoendana kile alichotarajia kukiimba kwa hadhira yake. Anasisitiza kutaka kuwaingiza wakristo kwenye

matendo ya kumuabudu Mungu kwenye shuhuli zao za kila siku. Anakariri “kutaka kuingiza” huku na kukusifu kuwa ni kwa manufaa ya kubarikiwa na kuteuliwa ili kupata baraka za Mwenyezi Mungu.

Kutokana na tafsiri ya kamusi ya ishini na moja toleo la nne, neno “kuingiza” limetokana na kuambishwa kwa kitenzi “ingiza” linalomaanisha kuongoza kitu au kiumbe kuingia mahali palipo ndani. Anwani ya nyimbo inaibua fikra tofauti na hata pale anapoikariri sehemu hii peke yake kwenye wimbo husika. Hali hii inazua maswali kwenye kujiuliza hasa nia ya wimbo huu ni kuzua fikra gani haswa.

Nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma tukiziorodhesha kwa kuzipanga kwa njia ya kinasibu kulingana na wakati alipozirekodi zinazua hisia na fikra tofauti kabisa. Hebu tazana orodha hii ya anwani ya nyimbo zake: *Ingia Ndani*, *Tuko Uchi*, *Napenda Mbele, Yesu Ninyonye, Imesimama, Nataka Nikuingize, Bend This Way, Yesu Panua, Yesu Nimwagie* na *Ni Tamu*.

Orodha hii ya nyimbo za msanii huyu husika inadhihirisha mpangilio wa kimakusudi kwani ameipanga kwa kurejelea hatua zote zinazoshirikishwa na mchakato mzima wa tendo la ndoa kulingana na uteuzi wa msamiati alioutumia kwenye anwani za nyimbo zake.

## 4.6 Athari za Mtindo wa Msuko wa Maudhui na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma

Athari kutokana na maelezo ya tafsiri yake ni mabadiliko yanayoletwa na mtu au kitu kwa mtu au kitu kingine kwa sababu ya mwingiliano wa vitu hivyo viwili kwa kiawango fulani. Maudhui kwa upande mwingine ni ujumbe wa pamoja ambao unajitokeza kwenye fasihi ya kazi na hujumuisha mafunzo yanayopatikana humo.

Mtindo ni ule upekee wa kazi ya fasihi unaomdhihirisha na kumtofautisha mtunzi wa kazi hio husika na utunzi wa kazi zingine za kifasihi.

Msuko kulingana na Wamitila (2008) ni mpangilio wa matukio kiusababishi katika kuijenga ploti ya kazi ya fasihi. Katika mchakato mzima wa kuyajenga maudhui ya kazi ya fasihi kama nyimbo ambapo maneno hutumika, sharti pawe na dhamira ya kiusababishi katika kuyateua maneno ili kusuka maudhui ya kazi husika.

Uteuzi huu wa maneno sharti utiririshe maudhui hayo kama uteuzi wa maneno yaliyochaguliwa na kuzua maudhui kwa njia ambayo haitaleta mkanganyiko kwa njia yoyote wa kimaana. Tukiangazia atahri za mtindo wa kusuka maudhui na matumizi ya lugha, tumeegemea mihili yote miwili ya nadharia ya simiotiki. Tutaegemea mhimili wa ishara unaoshorikisha ujenzi wa maana ya neno kulingana na uhusiano wa kinasibu na pia kuegemea mhimili wa pili wa kitaja na kitajwa. Hapa tutaegemea zaidi kwenye misimbo ya: Kihemetiki unaoegemea upataji wa maana kutokana na anwani ya kazi ya fasihi, Kiseme unaegemea upataji wa maana ya maneno yaliyotumiwa katika kazi ya fasihi kwa njia ya kutafsiri maana ya ndani ya kimafumbo yenyewe na Kiutamaduni ambapo maana ya maneno yaliyotumika kwenye kazi ya fasihi huegemea na viashiria vya kitamaduni ya jamii fulani. Misimbo hii tunaitumia na kuigemea kwa kiasi kikubwa ili kupata athari zinazojitokeza kwa hadhira.

Katika kuangazia athari za mtindo wa kusuka maudhui na matumizi ya lugha, nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma zinazua athari chanya na hasi.

Mount Kenya University

### 4.6.1 Athari Chanya kwenye Mtindo wa Msuko na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma ni kama zifuatazo:

#### 4.6.1.1 Kueneza Injili

Kueneza Injili kama ilivyoangaziwa katika Agano Jipya kwenye kitabu kitakatifu cha Biblia ni ile hali ya kutangaza matendo ya Mungu miongoni mwa wanadamu. Matendo haya yanahusisha miujiza na hata kuishi maisha matakatifu.

Kulingana na tafsiri ya Kamusi ya Karne ya Ishirini na moja, neno Injili linatafsiriwa kama maandishi yenye mafunzo ya kidini katika sehemu ya Biblia yaliyoandikwa na wanafunzi waliokuwa wanaambatana na Yesu.

Nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma kama *Imesimama, God Is Good, Injili Ni Tamu na Yesu Nimwagie*, zote hizi zinasimulia mambo ya miujiza na jinsi Mungu anavyopenda wateule wake waishi kiungu.

Katika wimbo wa *Imesimam*a anakariri maneno kama "......Injili imesimama......", akinuia kutilia msisitizo wa jinsi neno la Mungu lilivyo thabiti na kwamba halibadiliki. Katika kukariri haya, anaendeleza maudhui ya ukuu wa Mwenyezi Mungu kwenye wimbo na kuufikisha ujumbe kwa hadhira vyema. Maudhui haya yanamuathiri msikilizaji wa nyimbo zake moja kwa moja kwenye mtagusano wake na matendo ya Mungu kwenye maisha yake.

Katika kuyakariri maneno kama "Injili imesimama" anatilia mkazo kwenye kumtia muumini imani ya kumtumainia Mungu kwenye kungoja mipango ya Mungu. Mipango hii anaitumania muumini sharti awe na imani ya kwamba Mungu ndio tegemeo lake kama ilivoandikwa kwenye vitabu vilivyoanadikwa na wanafunzi wa Yesu vya Injili.

Kwa kusikilizwa kwa nyimbo hii husika, hadhira yake inajenga misingi na kupata matumaini ya kikristo amabyo bila shaka husheheni matendo ya kimiujiza na utoaji wa shuhuda kila panapo haja.

Katika wimbo wa *God Is Good* anazidi kariri maneno haya, "........God Is Good all the time......" ambayo katika kuyatafsiri kisisisi yanamaanisha ".....Mungu ni mwema kila wakati..." Katika shuhuli za kueneza injili, matendo ya Mungu ya kimiujiza hushirikishwa na kuenezwa kwa waumini ili kuwapa matumaini maishani, jambo hili ndilo linalotiliwa mkazo zaidi kwenye kukariri maneno haya husika katika wimbo huu.

Kama Yesu alivyowaagiza wanafunzi wake baada ya kupata roho mtakatifu, aliwaamuru kwenda kulitangaza neno na la Mungu na kutenda miujiza, muiongoni mwa miujiza hio ni kuponya wagonjwa na uutangaza ukuu wa Mungu kwa mataifa. Matendo kama ilivyotafsiriwa kwenye Kamusi ya Ishirini na moja yanachukua dhana ya moja moja ya matemdo ya kueneza injili.

Christopher Nyangwara Mosioma katika kuusifu ukuu wa Mungu na sifa zake kwenye wimbo huu ni wazi kwamba hadhira ya nyimbo zake zinapata kuyajua matendo ya Mungu na hata kuyatolea ushuhuda miongoni mwao.

Wimbo aliouita *Injili Ni Tamu* unaendana moja kwa moja na athari hii ya kueneza injili. Ikimbukwe kwamba matendo ya kiinjili husisitiza zaidi matendo mazuri na ya kimiujiza miongoni mwa bidamu. Ni katika matendo haya ambapo muumini anafurahia baraka yake na kuineza na hata kuitolea ushuhuda mbele ya waumini wengine. Mchakato wa kupokezana ujumbe huu wa ukuu wa Mungu miongoni mwa waumini ndipo injili inavyojipata kuenea na kutapakaa kama moto nyikani.

Injili pia inaenezwa kwenye wimbo uitwao *Yesu Nimwagie*. Ukuu wa Mungu unaendelea kuenezwa kwa kumsifu na kumtukuza na kubainisha sifa hizi hata kuzisema kwamba ndege wanazijua. Ukuu wa Mungu anaouongelea kwenye wimbo huu anautilia chuku na kuusema kwamba ndege wanauimba kila uchao. Mtindo huu unashirikisha kuenezwa kwa injili na hata ndege wa mwituni.

### 4.6.1.2 Kujenga Matumaini miongoni mwa Waumini

Dhana ya kujenga matumaini hurejelea hali ya kuwa na mtazamo chanya kwamba mambo yako yatakuendea vizuri baada ya kipindi fulani cha kuvunjika moyo. Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma anadhihirisha dhana hii katika nyimbo zake kama: *Imesimama, Ingia Ndani, Nataka Nikuingize* na *Bend This Way*.

Katika wimbo wa *Imesimama* anasema, "*.........barogi mbakonyetangaa*....." kwa lugha ya Ekugusii inamaanisha "wachawi hawawezi isamisha......" akikariri uwezo aliyonao Mwenyezi Mungu kwamba lolote apangalo haliwezi kubadilishwa na chuki ya binadamu. Anajaribu kumhimiza mwanadamu kuwa na imani kwa Mungu na kwamba shida ni za muda tu kwani Mungu ana mipango mizuri nasi.

Kama inavyotafsiriwa na kamusi ya karne ya ishini na moja toleo la nne, neno tumaini limepachikwa na dhana ya kuwa na imani kuwa upo uwezekano wa kufanikiwa au kupatikana kwa jambo fulani.

Wimbo kwa jina *Ingia Ndani* anaendelea kusema, ".......our Redeemer is the king of universe....." kwa utafsiri sisisi "......muhuishi wetu ni mfalme wa ulimwengu......" akiendeleza kukariri kwamba Mungu ana uwezo wa kubadilisha mambo kwa kuvuva na kwamba yeye ndiye mwenye uwezo mkubwa duniani na kwa hivyo tumtumainiye yeye.

Kwenye wimbo wa *Nataka Nikuingize* anasema, "...........hata nikiinama....nikiinuka mbele nyuma napata raha akiwa ndani......" akimaanisha hata akipata shida za kumvunja moyo ana imani kwamba shida hizo siza milele kwani Yesu yu ndani yake na atamaliza madhila hayo. Anaendeleza matumani maishani anaposema "......bisha utafunguliwa......." katika wimbo wa *Bend This Way* akirejelea kwamba unapokuwa na matatizo na umute Mungu lazima ataitikia mwito na atakupa uombalo.

Nikiangazia athari hasi kwenye mtindo wa msuko na matumizi ya lugha katika nyimbo za Injili za msanii husika ni kama zifuatazo:

### 4.6.2 Athari Hasi kwenye Mtindo wa Msuko na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma ni kama zifuatazo:

#### 4.6.2.1Mkanganyiko wa Kimaana kwa Hadhira

Mkanganyiko ni hali ya kutokuwa na uhakika wa mambo haswa pale ambapo kuna hali ya ati ati na sintofahamu ambazo zinapelekea hali hio. Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma kuna hali ya mkanganyiko wa kimaana katika mchakato mzima wa kusuka madhui na matumizi ya lugha kwa sababu ya uteuzi wa maneno yanayozua utata kwenye maana hasa katika kuyakariri kwenye nyimbo husika.

Hali hii inajitokeza katika nyimbo: *Yesu Nimwagie, Imesimama, Nataka Nikuingize, Napenda Mbele, Yesu Panua, Tuko Uchi na Yesu Ninyonye*.

Kama inavyobainika wazi kwenye anwani za nyimbo zote hizi, kuna hali ya si ntofahamu ya maana ya uteuzi wa maneno ya anwani hizi. Katika hali ya maana ya maneno lazma pawe na dhana inayowasilishwa na neno husika na dhana hii inaweza kubadilika kulingana na mtazamo wa jamii au hata katika matumizi ya kimaana kwenye kigezo cha umri na hata mandhari.

Tukiangazia wimbo alioupachika jina "*Yesu Nimwagie*," analeta sintofahamu kutokana na matumizi ya neno "Nimwagie" katika lugha ya vijana. Kama ilivyodesturi katika lugha ya kiswahili ya kuambisha vtenzi; neno "nimwagie" limezalishwaa na kuambishwa kwa neno "mwaga" linalotafsiriwa na kamusi ya karne ya ishirini na moja toleo la nne kama kutoa kitu cha majimaji, punjepunje au unga ndani ya kitu kingine na kukitawanya.

Kulingana na alivyokusudia tukiegemea dhima ya nyimbo za Injili, Chrstopher Nyakwara Mosioma alilitumia ili kusisitiza dhana ya kutumaini kumiminiwa baraka na Mwenyezi Mungu. Wingi huu wa baraka hizi ndio uliompelekea yeye kuuwekea dhana ya kumiminiwa ili kusisitiza ukuu wa Mungu.

Kwa upande mwingine tukiegemea msamiati wa lugha ya vijana neno "nimwagie" linahusishwa na dhana tofauti kabisa. Neno hili husika limepachikwa dhana ya kingono inayorejelea kufika kileleni kwa mwanaume wakati wa tendo la ndoa. Tafsiri hii inawepekelea vijana kuwa na mawazo potofu kabisa kwenye kuuimba wimbo huu kinyume na dhima ya utunzi na uimbaji kwa nyimbo za kidini.

Neno lingine la utata ambalo Christopher Nyangwara Mosioma alilikariri kwenye wimbo wake mmoja  na kuleta mkanganyiko wa kimaana ni "imesimama," kwenye wimbo *Injili Imesimama*. Tukiangazia kinachoimbwa na kusisitizwa kwenye wimbo huu huku tukiegemea kwenye dhima ya nyimbo za kidini, tunapata kurejelewa kwa uwezo na ukuu wa mipango ya Mungu ambayo haiwezi kugeuzwa na mtu yeyote yule. Dhima hii ina kuza kwa kiwango kikubwa maudhui ya ukuu wa Mungu na matendo yake yasiyokuwa ya kufananishwa na ya yeyote yule.

Kulingana na tafsiri ya Kamusi ya karne ya ishirini na moja toleo la nne neno "simama" limetasiriwa kumaanisha kuwa wima kwa kutegemea miguu au kitako cha kitu yaani kuinuka.

Kwa upande mwingine neno hili kulingana na matumizi na tafsiri ya lugha ya vijana huku nikiegemea miktadha yao ya matumizi, wanalitumia kuleta dhana ya kuwa tayari kwa uume wa mtu ili kwa nia ya kufanya tendo la ndoa; kusimika.

Christopher Nyakwara Mosioma analeta mkanganyiko kwenye matumizi yake ya neno hili kwa kulikariri likiwa peke yake katika korasi ya wimbo husika na kuwalimbikizia vijana hisia za kingono wanaposikiliza wimbo wenyewe kinyume na kusudi na dhima ya nyimbo za Injili.

Mkanganyiko mwingine wa maana ya baadhi ya msamiati aliyouteua Christopher Nyangwara Mosioma  anauendelea kwenye wimbo wake mwingine aliyouita "*Nataka Nikuingize*." Wimbo huu ameupachika msamiati unaoendana na kile alichotarajia kukiimba kwa mashabiki wake. Amedhamiria kwa upande mmoja kuleta dhana ya kunuia kuwaingiza wakristo ndani ya matendo ya kumuabudu Mungu kwenye shuhuli zao za kila siku. Embarambamba anarudiarudia "kutaka kuingiza" huku na kukulimbikizia sifa kuwa ni kwa ajili ya faida ya kupata baraka au hata kuchaguliwa kwa kusudio la kutabaruku baraka za Mwenyezi Mungu.

Tukiangazia tafsiri ya kamusi ya ishirini na moja toleo la nne, neno "kuingiza" ambalo limetokana na kuambishwa kwa kitenzi "ingiza" linaleta dhana ya kuongoza kitu au kiumbe kuingia mahali palipo ndani. Anwani ya wimbo huu inaibua hisia na fikra chafu hasa pale anaporudiarudia sehemu hii pekee yake kwenye wimbo husika. Hali hii inazua maswali kwenye kujiuliza hasa nia ya wimbo huu ni kuzua fikra gani haswa.

Hali ya mkanganyiko wa kimaana unaendelea kujitokeza kwenye kuyateua maneno ya anwani ya wimbo aliyouita " *Napenda Mbele."* Tukiangaziamuktadha wa matumizi kama alivyokusudia Christopher Nyankwara Mosioma, alikusudia kueleta dhana ya kujipiga jeki kiuchumi na hatimaye kuwa mja mwenye kipato miongoni mwa watu. Anaitilia shime dhana hii ya kupanda

ngazi kiuchumi anapotoa sababu ya "kupenda mbele" kwake ni kwa kuwa " nyuma" kuna vumbi na madharau. Kama nilivyotanguliza hapo awali kauli hii inadhihirisha bayana dhana ya kupata dharau na mateso hasa pale ambapo mja anapokuwa hana uwezo wa kiuchumi na hata mchafu wa mwili.

Maneno haya mawili yakichanganywa pamoja yanaleta mkanganyiko wa kimaana kwenye matumizi yake katika lugha ya vijana. Dhamira kuu ya msanii huyu katika kutumia msamiati wa lugha ya vijana ni kuwavutia na kuwanasa kwenye kusikiliza nyimbo zake, lakini kwa upande mwingine ni hatua inayoleta utatanishi kwenye kuuelewa wimbo huu huku tukiangazia zaidi kwenye ujumbe unaodhihirishwa na anwani ya nyimbo wenyewe. Kulingana na tafsiri na wanavyoifasili anwani ya wimbo huu husika ni kwamba "kupenda mbele" kunahusishwa moja kwa moja na dhana mja kupenda tendo la ngono. Fasili hii inaleta sintofahamu hata kwenye kiwango cha lugha ya adabu na heshima kilicho kwenye nyimbo za Embarambamba.

Christopher Nyangwara Mosioma anaendelea kutumia msamiati unaoleta mkanganyiko hasa tukiegemea lugha ya vijana kwa kuupa anwani wimbo wake mwingine kwa jina " *Yesu Panua*." Kulingana na kusudio lake kwenye muktadha wa mazingira ya matumizi ya maneno haya katika wimbo huu, msanii huyu ananuiia kudhihirishaa dhana ya kujiendeleza kimapato na kuwa na upana mrefu wa kiwango cha kifedha kama nilivyotanguliza kusema mwanzoni.

Sintofahamu inatokea tu pale ambapo analikariri neno " panua" mara kadhaa likiwa peke yake na kuzua fikra potofu miongoni mwa hadhira yake lengwa ambayo ni vijana. Anaendeleza mkanganyiko zaidi anapokariri maneno haya:

*"...........nataka nikugonge........ panua nikugonge....."*

Kama nilivyoangazia hapo awali, tafsiri ya kamusi ya karne ya ishirini na moja toleo la nne, neno "Panua" linamaana ya kufanya kuwa kubwa kwa upana au kuongeza kwa nia ya kutanua.

Tafsiri inayoendana moja kwa moja na tafsiri ya lugha ya vijana ambao mara nyingi kwa mitazamo yao, lugha zao husheheni usamiati mwingi wa kurejela dhana zilizofumbwa kimaana na zenye kusheheni mambo machafu. Msamiati huu wa kurejelea vitu vichafu kimaadili hutumia maneno ya kawaida ili kuficha ukali wa kile wanachorejelea na wala hautimii maneno ya tasfida za kawaida.

Kwa maalezo haya, neno panua kama lilivyoelezwa na kamusi ya karne ya ishirini na moja, vijana wanalitumia neno hili kurejelea dhana ya kuweka mguu wa kulia na kushoto kuwa mbali na mwingine kwa nia ya kuruhusu kupenyezwa kwa utupu wa kiume kwenye utupu wa kike. Hivyo basi kwa kuegemea dhana hii ya tafsiri hii ya vijana, mtindo alioutumia Christopher Nyangwara mosioma wa urudiajirudiaji wa neno hili pekee yake kwenye wimbo husika unawazamisha vijana kwenye fikra na mawazo ya kingono kinyume na kuwekwa kwenye mawazo ya kitakatifu na ya kiungu.

Fikra za kingono zinaendelea kusheni na kuhusishwa na nyimbo za Christopher Nyakwara Mosioma kwenye wimbo aliyouita "*Tuko Uchi*." Kama inavyoelezewa katika tafsiri ya kikawaida kwenye kamusi ya Kiswahili ya karne ya ushirini na moja Toleo la nne, neno " uchi" linafunganishwa na dhana inayorejelea hali ya kutokuwa na nguo na kuwa kama mtu alivyozaliwa, yaani kuwa tupu. Dhana hii pia hutumiwa katika matumizi ya kinahau kama vile kwenye nahau inayosema "kuvuliwa nguo hadharani" ; inayorejelea dhana ya kuaibishwa au kutiwa aibu hadharani kwa lengo la kumdhalilisha mtu.

Tukiegemea dhamira ya msanii Christopher Nyangwara Mosioma iliyompelekea kutumia maneno haya, tunapata aiyatumia kijazanda kuelezea jinsi ya vile tunavyoonekana mbele za mwenyezi Mungu, hii ni kulingana na tunayoyafanya ambayo aghlabu huwa kinyume na mafundisho ya Mungu. Msanii huyu alinuia kuendeleza maudhui ya ukuu wa Mungu ambao kulingana na sifa hii ana uwezo wa kuyafahamu mabaya yote ambayo tunayafanya kwa njia ya siri huku tukidhania hakuna yeyote anayetuona.

Kwa upande mwigine uteuzi wa maneno haya katika nyimbo za injili tukiegemea kwenye sifa, mazoea na desturi katika sajili ya kidini, uumbaji wa anwani hii unakengeuka kabisa sifa hizo. Tukiegemea kwenye ukweli  kwamba kati ya sifa za msamiati wa kidini ni kusheheni kwa maneno ya heshima na adabu. Anwani hii katika mazingira ya utafsiri wa kawaida inaleta na kuzua athari ya kutia aibu na kuvunja miiko hasa katika shuhuli za kiibada ambazo hushirikisha watu wa umri tofauti tofauti bila kubagua watoto. Kwa mtazamo huu kulingana na tamaduni na desturi za jamii, dhana ya watu kuwa uchi inaposhirikiswa kwenye shuhuli za kiibada inaweza kuleta kuhamishwa kwa fikra za kiungu na kuletwa kwa fikra za hali ya kidunia ya anasa iwapo kutatoweka umakini na uzingativu  wa uelewa wa kinachozungumziwa.

Nikimalizia kuangazia nyimbo zinazoibua mkanganyiko wa maana za msanii huyu husika, nitaangazia uteuzi wa maneno aliyoyachagua kuumba anwani ya wimbo aliyouita "*Yesu Ninyonye*." Maneno haya kama nilivyoeleza hapo awali, alidhamiria kuyatumia kijazanda. Christopher Nyangwara Mosioma alikusudia kuleta na kuzua dhana ya kusamehewa na kuwa msafi wa dhambi ( "kunyonywa" ), alidhamiria kuibua kutojalishwaa na kiwango cha idadi ya matendo yaliyosheheni dhambi ambayo mja ameyafanya. Kulingana na maudhui aliyoyalenga kuyauza kwenye wimbo huu, alikusudia kufafanua jinsi Mungu alivyo na uwezo wa kufuta dhambi mara moja."Unyonyaji" wa dhambi hizi unakusudiwa kuonyesha uharaka na uwezo wa

kipekee wa kufanywa kwa jambo hilo hasa kwenye kuegemea ukuu na uwezo alionao Mwenyezi Mungu.

Katika upande mwingie tukiegemea tafsiri ya Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja toleo la nne, neno "nyonya" linafasiliwa kuleta dhana ya kitendo cha kuvuta kitu cha majimaji kwa kutumia mdomo, kama ndama au mtoto afanyavyo maziwa ya mama yake. Kwa kujikita kwenye maana hii iliyotafsiriwa kwenye kamusi kunaibuka utata katika tafsiri ya vijana kwenye matumizi yao ya neno hilo.

Kulingana na matumizi na muktadha wa lugha ya vijana kama wanavyolitumia neno hili, dhana inayosimamiwa na kupachikwa nao ni ile ya kuashiria kufyonza chuchu na hata utupu wa mpenzi wako ili kumuandaa kwa tendo la ndoa. Mwimbaji Christopher Nyangwara Mosioma anarudiarudia neno " kunyonywa" kwenye korasi ya wimbo huu husika kwa madhumuni ya kuinasa hadhira yake kwenye kusudio tofauti na kile walichozoea kupachika kwenye tafsiri ya neno hili.

Fikra chafu na za kingono zinasheheni kwenye kuimba na kuusikiliza wimbo huu pale anapotumia mtindo wa urudiaji wa neno hili husika. Anawafanya wasikilizaji wa nyimbo zake kupata burudani hasi ya fikra hasa pale wanapojua walichozoea kudhania kwenye maana ya neno hili si kile kinachoimbwa na msnii husika jambo linalowapelekea kufanya mzaha wanapouimba wimbo wenyewe. Mzaha huu ndio unaoleta athari hasi kinyume na dhima ya nyimbo za injili ambazo hufungamanishwa na mambo ya kidini.

Athari hii inaambatanishwa na fikra za kingono na chafu ambazo hupelekea kutosikilizwa nyimbo hizi mbele ya mihadhara ya dini ya wakristo ilhali wao ndio 'walengwa" haswa wa nyimbo hizi.

#### 4.6.2.2 Kubadilisha Dhamira Kuu ya Nyimbo za Injili

Dhamira katika kazi za fasihi ni lile lengo au shabaha ya kazi husika kunuia kuafikia baada ya kazi hio kuwasilishwa kwa hadhira lengwa. Kama kawaida nyimbo za dini huwa na dhamira ya kulitukuza jin la Mwenyezi Mungu na kuwapa waumini matumaini kwenye maisha yao. Malengo aghalabu huweza kudhihirika wazi kuanzia kwenye anwani ya nyimbo yenyewe na kutiliwa mkazo kwa ukariri wa korasi.

Katika kuziumba anwani na hata korasi za nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma hali haijitokezi wazi bali kuzua hisa mseto na hata aibu iwapo utarejelea anwani za baadhi ya nyimbo zake. Nyimbo zenyewe ni pamoja na *Yesu Nimwagie*, *Imesimama*, *Nataka Nikuingize*, *Napenda Mbele*, *Yesu Panua, na Yesu Ninyonye*.

Nikianza kuangazia wimbo wa *Yesu Nimwagie* kutoka kwa anwani yake, fikra zinazomjia msikilizaji kutokana na uteuzi wa msamiati wa kuumba anwani hii zinaweza kuwa kwa kiasi fulani ziwe na kingono. "kumwaga" kama nilivyoangazia hapo awali ni dhana inayoeleweka na vijana kama kufika kileleni katika tendo la ndoa.

Katika wimbo aliyouita *Imesimama*, bado kuna kupachikwa kwa fikra za jingono kwa asilimia fulani. Kulingana na dhana ya lugha ya vijana na kwa matumizi ya kawaida ya kitafsida, neno simama linaweza pia kurejelea dhana ya hali ya kuwa tayari kwa uume kufanya tendo la ndoa.

Mbali na neno "kuingiza" kuwa na maana ya kutumbukiza kitu ngani ya kingine kilicho na mwanya, pia lina beba dhana ya kutia uume ndani ya uke. Tafsili hii inapochipuza kwenye nyimbo za kidini na hasa za injili huleta mkanyiko wa dhamira ya mtunzi.

Mkanganyiko huu pia wa dhamira unachipuza pale Christopher Nyakwara Mosioma alipotumia msamiati kama "napenda mbele" kwenye kutengeneza anwani ya wimbo. Maneno haya yanauwezo mkubwa wa kuzua fikra za kingono na kuleta dhana ya mtu "kupenda tendo la ndoa."

Kulingana na maneno aliyoyatumia kwenye kusuka msamiati wa wimbo aliyouita "*Yesu Panua,"* msanii huyu anaendelea kuzua fikra za kingono kwnye nyimbo zake. Hebu tazama maneno haya:

> *"................nasikia nikugonge......iiih panua...eeeh panua.....sasa panua nimeanza kazi......"*

Kulingana na mpangilio wa hatua hizi na matumizi yanayoegemea lugha ya vijana, maneno haya yanaegemea sana mammbo ya ngono kuliko ya kumtukuza Mungu.

Fikra za kingono zinatawala msikilizaji wa nyimbo za Christopher Nyakwara Mosioma hasa anapousikiliza wimbo aliouita "*Yesu Ninyonye."* Tazama msamiati huu unaopatikana kwenye wimbo wenyewe:

> *"........nataka kunyonywa pande zote........."*
>
> *"...............nataka kunyonywa pande zote........."*
>
> *"................sijui utaanzia wapi......."*
>
> *".............bora uninyonye.........."*
>
> *"........nataka kunyonywa sana sana............"*
>
> *"...............nitalala wapi uninyonye........."*

Msamiati huu kwa mtazamo wa mambo ya kimwili umesheheni matendo ya kingono na kujenga fikra chafu kuliko fikra za utakatifi kama zinavyofaa kudhihirishwa na nyimbo za injili.

Kama ilivyodhihirika wazi katika maelezo haya hapo juu ni wazi kwamba nyimbo nyingi za injili alizotoa Christopher Nyakwara Mosioma kati ya mwaka wa 2021-2023 zinasheheni fikra na dhamira za kingono zaidi kuliko dhamira za kumuabudu Mungu.

**4.6.2.3 Mawasiliano ya Kuaibisha**

Kama ilivyo katika kaida za jamii zozote duniani aghlabu za kiafrika, sharti pawepo na mawasiliano yanayoleta stara na heshima. Ijapokuwa wakati mwingine maneno yanayofaa kutumiwa huwa ya wazi wazi bila kificho na hapo ndipo hupelekea kuwepo kwa matumizi ya tasfida kwa minajili ya kuficha ukali wa maneno yenyewe.

Katika nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma, uteuzi wa maneno yake mengi yanawajaza wasikilizaji wa nyimbo zake na fikra zilizojaa uozo na aibu. Fedheha hii huchipuza kwa kiasi kikubwa kwenye kuegemea maana yake ya kawaida na matumizi ya kila siku ya lugha za vijana na hata matumizi ya kawaida katika jamii.

Hebu tazama uteuzi wa maneno haya kama alivyoyatumia msanii huyu katika anwani za nyimbo zake za Injili; *Tuko Uchi, Yesu Ninyonye, Imesimama, Napenda Mbele, Yesu Panua, Nataka Nikuingize, Ingia Ndani* na *Yesu Nimwagie*.

Ikumbukwe kwamba maneno haya ndiyo yanayokaririwa katika nyimbo hizi teule kuanzia mwanzo wa nyimbo hadi mwisho. Msamiati huu ndio unaotumiwa kwa kiwango kikubwa na vijana kurejelea masuala yanayohusiana na ngono. Usikilizaji wa nyimbo hizi teule huleta aibu miongoni mwa wasikilizaji iwapo hakuta kuwa na umakini wa kuelewa kinacho zungumziwa katika nyimbo zenyewe.

Uteuzi wa msamiati wa aina hii ya maneno umesheheni hatua za kufanya tendo la ndoa kuanzia kwenye maandalizi hati kileleni mwake. Ama kweli nyimbo hizi zinatia aibu kwenye kuziimba na hata kuzitaja mbele ya watu wanaoimudu vyema lugha husika.

## 4.7 Hitimisho

Sura hii imeangazia uchanganuzi wa data na ufasiri wa matokeo ya utafiti. Kwanza kabisa historia fupi ya msanii husika iliangaziwa na badae muhtasari wa kazi za msanii huyo ziliangaziwa kwa kina. Kama ilivyobainika wazi katika utafiti huu, sura hii imeangazia uwasilishaji wa matokeo ya utafiti ambayo yalihusisha maudhui anayoyaangazia msanii Christopher Nyangwara Mosioma katika nyimbo zake za Injili na uteuzi wake wa matumizi ya lugha katika msuko wa kazi zake na kutathmini athari zake kwa hadhira. Baada ya kukamilisha kuichanganua data na kutoa matokeo ya utafiti, sura inayofuata imejadili muhtasari wake na mapendekezo yanayotokana na kazi hii.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii itaangazia muhtasari wa utafiti huu, matokeo yake, mapendekezo na kumalizia na hitimisho ili kukamilisha kazi hii.

### 5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulinuia kuangazia Mtindo wa Nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma katika mwaka wa 2021-2023.

Kazi hii iliongozwa na malengo matatu ambayo yalimsaidia mtafiti kuufanya utafiti huu kwa njia mwafaka. Malengo yenyewe yalihusisha kuainisha msuko wa maudhui katika nyimbo za Christopher Nyangwara Mosioma Mosioma (*Embarambamba*) pamoja na kuchanganua matumizi ya lugha ya kisanaa katika nyimbo za msanii husika kati ya mwaka 2021- 2023 na kumaliza na lengo na tatu lililoshirikisha kutathmini Athari za mtindo wa msuko wa maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo husika.

Katika mgao wa mambo yaliyoshuhulikiwa na utafiti huu, kazi yenyewe iligawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza iliangazia usuli wa mada ambapo hoja kadhaa kuhusu mada iliyochaguliwa kufanyiwa utafiti zilijadiliwa. Suala la utafiti pia liliangaziwa katika sura hii ambapo malengo matatu ya utafiti wenyewe yalifumwa ili kujibu maswali ya utafiti yaliyochipuka kuongoza, kujibu na kufanikisha utafiti wenyewe. Katika kumalizia sura hii ya kwanza umuhimu wa utafiti uliangaziwa ambapo upeo na mipaka ya utafiti wenyewe ukiwekwa wazi. Maelezo ya Istilahi zilizotumika katika hoja za sura hii pia ziliangaziwa humo.

Sura ya pili iliangazia mwauo wa mwandishi na yaliyoandikwa kuhusu mada. Sura hii pia iliangazia nadharia iliyotumika katika kuchanganua data na misingi ya nadharia yenyewe

ilielezwa kwa kina.Nadharia iliyoteuliwa ilikuwa ya Simiotiki iliyoasisiwa na Ferdnand Dessaussure. Sura ya tatu ya utafiti huu iliangazia muundo wa utafiti, sampuli na usampulishaji. Mbinu na vifaa vya kukusanya data pamoja na uchambuzi na uwasilishaji wa data ni mambo ambayo pia yalielezwa kwa kirefu katika sura hii na kumalizia na maadili ya utafiti wenyewe.

Katika sura ya nne, maelezo na historia ya msanii husika iliangaziwa. Iligundulika kwamba Christopher Nyakwara Mosioma alizaliwa mnamo mwaka wa 1988 mjini Keroka na badae kupachikwa jina la *Embarambamba* kutokana na weledi wake wa upigaji ng'oma. Ilibainika wazi kwamba kabla kuanza kuimba nyimbo za Injili, msanii huyu alikuwa akiimba nyimbo za kiulimwengu. Mambo yaliyochipuka kutokana na uchanganuzi wa data yalijadiliwa na kufafanuliwa kwa uwazi.

Ni dhahiri shahiri kuwa nyimbo za Injili za Christopher Nyangwara Mosioma ziliibua maudhui kadhaa kama: Maendeleo ya kiuchumi ambayo yalizuka wazi kwenye nyimbo; *Bend This Way, Napenda Mbele*, *Nataka Nikuingize*, *Nataka Kunyonywa* na *Yesu Panua*. Maudhui mengine yaliyozuka yalikuwa ya Ulokole yaliyodhihirika kwenye nyimbo; *Ingia Ndani, Imesimama, Nataka Nikuingize, God Is Good* na *Nataka Nikuingize.* Imani ya kidini ni maudhui yaliyojiweka wazi kwenye nyimbo; *Bend This Way, Nataka Nikuingize, God Is Good, Yesu Nimwagie* na *Nataka Kunyonywa.* Nikitamatishia katika maudhui ya kudhihirisha Ukuu wa Mungu ambayo yalijidhihirisha wazi kwenye nyimbo alizozipa anwani: *Bend Ths Way*, *God Is Good*, *Tuko Uchi, Yesu Nimwagie*, *Nataka Kunyonywa* na *Yesu Panua.*

Mtindo uliojitokeza kwenye nyimbo hizi za msanii husika ulijumuisha matumizi ya takriri ambapo maneno kadhaa yalirudiwarudiwa katika nyimbo zake haswa katika kiitikio na vifungu bainishi kwenye nyimbo zenyewe. Iliabainika wazi kwamba kulikuwa na matumizi ya

kuhamisha na kuchanganya ndimi ambapo lugha za Kiswahili, Kiingereza na hata Ekigusii zilitumika.

Mtindo wa ulinganishi pia ilijitokeza ambapo kulikuwa na matumizi ya Tashbihi pale ambapo ulinganisho wa vitu au mambo mawili au zaidi kutumia maneno ya ulinganishi ulibainika na hata Istiari ziliibuka pale ulinganisho ulipojitokeza wa moja kwa moja. Unukuzi kutoka vitabu vitakatifu pia ulidhihirika wazi pale ambapo hadithi na visa kutoka kitabu cha Biblia zilionekana kwenye nyimbo husika na hata baadhi ya maneno kwenye nyimbo hizi yalidondolewa moja kwa moja kutoka kwenye Biblia.

Ilibainika wazi kwamba matumizi ya mtindo wa Usimulizi yalitumika kusimulia hadhithi na visa hivi katika nyimbo zenyewe. Usimulizi huu ulisheheni jazanda na uteuzi mahususi wa maneno ili kubainisha wazi au kwa njia ya mafumbo alichokilenga msanii huyu.

Katika kuangazia athari za mtindo wa msuko wa mauudhui na matumizi ya lugha kuliibuka mikondo miwili ya athari hizi; athari chanya na athari hasi. Athari chanya zilidhihirika wazi katika vipengele viwili. Kipengele cha kwanza kilikuwa cha kueneza Injili, ambacho kilijikita kwenye athari za nyimbo kama; *Imesimama, God Is Good, Ni Tamu* na *Yesu Nimwagie.* Kipengele cha pili kilikuwa kuhusu kujenga matumaini miongoni mwa waumini, ambacho kiliangaziwa kwenye utunzi wa nyimbo; *Imesimama, Ingia Ndani, Nataka Nikuingize* na *Bend This Way.*

Athari hasi kwa upande mwingine zilikuwa kwenye vipengele vitatu. Kipengele hasi cha kwanza kilihusu mkanganyiko wa kimaana kwa hadhira, ambapo nyimbo kama; *Yesu Nimwagie, Imesimama, Nataka Nikuingize, Napenda Mbele, Yesus Panua, Tuko Uchi* na *Yesu Ninyonye,* ziliangaziwa. Kipengele cha pili kiliangazia kubadilisha dhamira kuu ya nyimbo za injili , athari

iliyojiweka wazi kwenye niymbo; *Yesu Nimwagie, Imesimama, Nataka Nikuingize, Napenda Mbele*, *Yesu Panua* na *Yesu Ninyonye.* Mawasiliano ya kuaibisha, kikawa ndicho kipengele cha tatu cha athari hasi kwenye nyimbo husika za msanii Christopher Nyakwara Mosioma (*Embarambamba*). Athari inayotokana na uteuzi wa msamiati uliobeba dhana chafu za kingono miongoni mwa wanajamii kwenye kubuni anwani na hata kwenye viitikio vya nyimbo zenyewe.

Sura ya tano imeangazia Muhtasari wa utafiti mzima kutoka sura ya kwanza mpaka ile ya mwisho. Ni humo ndimo mlimozungumziwa matokeo ya utafiti, mapendekezo na hata kuhitimisha yaliyozungumziwa.

## 5.2 Mapendekezo

Kulingana na yaliyoibuka kutokana na utafiti huu, yafuatayo ni mapendekezo kwa utafiti wa mbeleni:

Kwanza, utafiti huu umemrejelea msanii Christopher Nyangwara Mosioma, hivyo utafiti mwingine unaweza fanyika baadae kwa kuangazia mtindo katika nyimbo za wasanii wengine.

Pili, katika utafiti huu tumejikita katika utanzu wa nyimbo, hivyo tunapendekeza kwamba utafiti wa badae unaweza kufanyika kwa suala kama hili kwa kurejelea tanzu nyingine za fasihi kama vile ushairi, hadithi, tamthilia na hata riwaya.

Tatu, utafiti huu ulitumia nadharia ya Simiotiki, hivyo basi tunapendekeza kwamba nadharia nyingine inaweza kutumika katika kulirejela suala hili la utafiti

Nne, utafiti mwingine unaweza kufanywa kuangazia athari za suala hili la utafiti ukiegemea kwenye kipengele cha jinsia au hata umri.

Tano utafiti mwingine unaweza kufanywa kwa kuegemea malengo tofauti na niliyoegemea kwenye utafiti huu.

Sita, mtafiti mwingine anaweza kufanya utafiti hata ikiwa kwa nyimbo za msanii mwingine akiegemea mbinu za ukusanyaji data na hata uchanganuzi wa data unaochukua njia tofauti na ile iliyoegemewa na utafiti huu.

## 5.3 Hitimisho

Sura hii ilishuhulikia Muhtasari wa matokeo ya uchanganuzi na shuhuli nzima ya utafiti na Mapendekezo ya mada ya utafiti kutokana na jinzi mtafiti alivyoyatoa. Mtafiti anaonyesha kuna jukumu la kila mmoja la kuteua maneno au msamiati mwafaka katika shuhuli zetu za mawasiliano ili kutunza heshima na kudumisha mawasiliano yenye adamu. Ni wazi kwamba katika mawasiliano yetu ya kila siku sharti pawe na uteuzi ufaao wa maneno ili kuufikisha ujumbe uliokusudiwa bila kileta maana kinzani.

Mount Kenya University

# MAREJELEO

Kothari, C. (1985). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi. Wiley Easton Limited.

Kingei, K. Na Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*: Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Jones, E. (1994). *Critical Theory of African Litarature Today*. London: James Curry Limited.

Katika ya Kenya (2010).

Gatambuki, M. (2010). *A cognitive linguistic analysis of Gikuyu Euphemisms*. (Haijachapishwa). M.A Thesis. Nairobi: Kenyatta University.

Fromkin, V. And Rodman, R. (1972, 1988). *An I ntroduction to Language (4th Edition*). Fort Worth: Holt, Reinhart and Winston.

Fowler, B. (1971). *The New Stylistics Style and Structure in Literature*. Blackwell: The Pitman Press.

Chiraghdin, S. And Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Kamusi ya Fasihi: Msingi na Vipengele vyake: Nairobi.

Brown, P. And Lewinson, S. (1978). *Politenes! Some Universal In Language Usage*. Cambridge. Cambridge Universal Press.

Brown, G. And Yule, G. (1983). *Disclosure Analysis*.Cambridge University Press.

Kamusi ya Fasihi: *Msingi na Vipengele Vyake*: Nairobi.

Farouk, M. (1974). *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Drabble, M. (1995) *The Oxford Companion to English Literature*, New York: Oxford University Press.

Kamusi ya Karne ya 21; Toleo la 4. Longhorn Publishera PLC.EMAC, BAKITA na KICD

Mount Kenya University

Wanyama, A. (2006). *Maudhui na Mtindo Katika Utendi wa Wabukusu "Khuswala Kumuse*.' Tasnifu ya M.A, Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wamitila, K. (2003b). *Kichocheo cha Fasihi; Simulizi na Andishi*, Nairobi: Focus Books.

Wandiba, S. (2010). J.M Kariuki: *A Biography. Nairobi Institute of Anthropology, Gender and African Studies.*

Wambua, M. (2001). *Mtindo wa nyimbo za Kikai Kilonzo*. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa). Kenyatta University.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Nisingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Oeri, W. (2012). *Musians In Court Over Hate Songs*. Daily Nation, 3rd July 2012. Pg 5.

Ochoi, P. (1998). *Uchunguzi Kimtindo Wa Ushairi wa Al-Amin Mazrui.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Senkoro, F. (2011). *Fasihi* Dar Es Salaam: TUKI.

Ngure, F. (2003). *Fasihi Simulizi Kwa Shule Za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mulokozi, M. na Kahigi, K. (1979). *Kunga Za Ushairi Na Diwani Yetu*. Dae Es Salaam T.P.H.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki ya Fasihi*. Nairobi: East African Educatinal Publications. *Kunga za Nathari Ya Kiswahili: Riwaya, tamthilia Na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, S. (1981). *Fanu Na Maudhui. Makala Katika Misingi Ya Nadharia Ya Fasihi*. Zanzibar. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Kur. 56-62 __________1995

De Genous, M. (2008). *Inmate, Relationship, Marriage and Families*. 7th Edition New York: Mc Grace Hill.

Chapman, R. (1982). *The Language of English Literature*. London: Edward Arnold Publishers.

Jifunze Utafiti: *Mwongozo Kuhusu Utafiti Wa Uandishi Wa Ripoti Wenye Mantiki*: Dar Es Salaam Ecumenical Gathering. (EGYS).

Mdee, J.(2006). *Nadharia na Historia Ya Leksikografia*. Dar Es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Lyons, J. (1995). *Language and Linguistics. An Introduction*. Cambridge University Press.

Lyons, J. (1981). *Language and Linguistics: An Introduction* Cambridge University Press.

Lyons, J. *Semantics Volume I*. Cambridge: Cambridge University Press.

Lyons, J. Semantics Volume II. Cambridge: Cambridge University Press.

Karanja, D. (2008). *Usawiri Wa Masuala Ibuka Katika Hadithi Za Watoto*. Tanifu ya Uzamili. Cho kikuu cha Kenyatta.

Habwe, J. (2005). Paradiso. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Lakoff, G. And Johnson, M. (2003). *Metaphors We Live*. By London: The UniversityOf Chikago Press.

Habwe, J. Na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Kearns, K. (2000). *Semantics Modern Linguistics*. Essex: Palgrare Macmillan.

Kearns, K. (2011). *Semantics*. Palgare: Macmillan Publishers.

Ogondi, B. (2005). *Uhakiki wa Usimamizi Katika Riwaya Ya Walenisi. Tasnifu Ya Uzamili*. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ntarangwi, M. (1990). *Maudhui Katika Nyimbo Za Remi Ongala*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Elihaki, Y. (2021). *Usanaa Wa Lugha Katika Ujenzi Wa Dhima Za Nyimbo*: Mfano kutoka Nyimbo Za Harusi Za Jamii Ya Waasu. Chuo Kikuu Cha Mtakatifu Agustino Cha Tanzania (SAUT).

Nkonge, M. (1988). *Literaly Study Of  Songs Of Josph Kimaru*. Theme and Style B.Ed Project. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Njogu, K.na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*, Nairobi: Jomo kenyatta Foundation.

Mwaniki, M. (2011). *Matumizi ya Lugha Katika Nyimbo Tohozi Za Salim Junior*. Tasnifu Ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mutwiri, G. (2005). *Mitazamo Ya Utendakazi Wa Nyiso Katika Jamii Ya Watigani*a. Tasnifu Ya Uzamili Chuo kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mohamed, S. (1995). *Kunga Za Nathari Ya Kiswahili.* East Africaan Educational Publishers. Nairobi.

Mertens, D. (1998). *Research Methods In Diversity With Quantitative Approaches*. AGE Publications. London.

Kothari, C. (2004). *Research Methodology: Methods And Techniques*. (2nd Edition). New Delhi: New Age International Publishers.

Manfred, J. (2005). *Narratology: A Guide To The Theory Of Narrative* Cologne: English Department, University Of Cologne.

Mount Kenya University

Lanser, S. (1981). *The Narrative Act Point Of View In Prose Fiction*. Princeton UP.

Mount Kenya University

# VIAMBATANISHO

Kiambatisho I : Barua ya idhini ya chuo (ERC)

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)**
Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

**The National Commission for Science, Technology and Innovation**, hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

**CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE**

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
   i. Endanger national security
   ii. Adversely affect the lives of Kenyans
   iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
   iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
   v. Adversely affect the environment
   vi. Adversely affect the rights of communities
   vii. Endanger public safety and national cohesion
   viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. The license any rights thereunder are non-transferable
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and
Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke

## Kiambatanisho II: Idhini ya Utambulisho

# Mount Kenya University

REF: **MKU/ISERC/4603**

Date: 19 November 2024

TO: **KIUNGA J. KESI**

REG: **MAKI/2019/60098**

Dear Sir/Madam,

**RE: MTINDO WA NYIMBO ZA INJILI ZA CHRISTOPHER NYANGWARA MOSIOMA (EMBARAMBAMBA) MWAKA 2021- 2023**

This is to inform you that **Mount Kenya University** has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is **3325.** The approval period is **19/11/2024 - 18/11/2025.**

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including informed consents, study instruments, MTA will be used
ii. All changes including amendments, deviations and violations are submitted for review and approval by **Mount Kenya University**
iii. Death and life-threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours of notification
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affect the safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions
vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal
vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to **Mount Kenya University**

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) https://research-portal.nacosti.go.ke and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely,

**Dr. Alfred Owino, PhD**
**Chairman, Mount Kenya University ISERC**

MOUNT KENYA UNIVERSITY
ETHICS REVIEW COMMITTEE
P. O. Box 342 - 01000,
THIKA

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Tel: +254 20 287 8000, Cell: +254 709 153 000
Email: info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke
Chartered and ISO 9001 : 2015 Certified

Kiambatanisho III: Barua ya Idhini (NACOSTI).

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 918657

Date of Issue: 29/November/2024

## RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Mr.. KIUNGA JONAH KESI of Mount Kenya University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Tanariver on the topic: MTINDO WA NYIMBO ZA INJILI ZA CHRISTOPHER NYANGWARA MOSIOMA (EMBARAMBAMBA) MWAKA 2021-2023 for the period ending : 29/November/2025.**

License No: NACOSTI/P/24/414303

**918657**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

National Commission for Science, Technology and Innovation -

**Kiambanatisho IV : Ripooti ya Turtin**

Mount Kenya University

# MTINDO WA NYIMBO ZA INJILI ZA CHRISTOPHER NYANGWARA MOSIOMA (EMBARAMBAMBA) MWAKA 2021- 2023

*by* Kiunga J. Kesi

**Submission date:** 30-Jun-2025 01:51PM (UTC+0300)
**Submission ID:** 2708328643
**File name:** PROJECT_TASNIFU_KESI_MAKI_final-2.docx (4.13M)
**Word count:** 23194
**Character count:** 132543

MTINDO WA NYIMBO ZA INJILI ZA CHRISTOPHER NYANGWARA MOSIOMA

(*EMBARAMBAMBA)* MWAKA 2021- 2023

**KIUNGA J. KESI**

TASNIFU HII IMETOLEWA 1 KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA

MTINDO WA NYIMBO ZA INJILI ZA CHRISTOPHER NYANGWARA MOSIOMA (EMBARAMBAMBA) MWAKA 2021- 2023

ORIGINALITY REPORT

| 11% | 10% | 2% | 5% |
|---|---|---|---|
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Submitted to Mount Kenya University<br>Student Paper | 1% |
| 2 | gospelgo.com<br>Internet Source | 1% |
| 3 | ir-library.mmarau.ac.ke:8080<br>Internet Source | 1% |
| 4 | ufufuonauzimamorogoro.blogspot.com<br>Internet Source | 1% |
| 5 | erepository.uonbi.ac.ke<br>Internet Source | 1% |
| 6 | journals.udsm.ac.tz<br>Internet Source | 1% |
| 7 | Submitted to Kenyatta University<br>Student Paper | <1% |
| 8 | Submitted to University Der Es Salaam<br>Student Paper | <1% |
| 9 | mapundagustaph.wordpress.com<br>Internet Source | <1% |
| 10 | repository.out.ac.tz<br>Internet Source | <1% |
| 11 | www.gotquestions.org<br>Internet Source | <1% |
| 12 | Submitted to Eiffel Corporation<br>Student Paper | <1% |
| 13 | www.prayerballoons.org<br>Internet Source | <1% |